

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**VERBATIM REPORT OF**

**CONSTITUENCY REPUBLIC HEARING**

**KIBWEZI CONSTITUENCY**

**AT P.C.E.A CHURCH**

**ON**

**14<sup>TH</sup> May 2002**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARING – KIBWEZI CONSTITUENCY ON 14<sup>TH</sup> MAY 2002 AT P.C.E.A  
CHURCH**

**Present:**

Com. Kabira  
Com. Zein Abubakar  
Com. Ahmed I.Hassan  
Com. Abida Ali

**Secretariat Staff in Attendance:**

Bi. Mwaimuna - Programme Officer  
- Asst. Programme Officer  
- Verbatim Reporter

**The meeting started at**

**Speaker:** Tarafa hii ya Kibwezi na Makindu. Kwa hivyo ningepomba Reverend wa hapa atuongoze kwa maombi, Reverend. Na aombe wale ambao wangali wanakuja.

**Reverend:** Ningetaka kwanza nawakaribishe katika kikao hiki chetu, hii inaitwa P.C.E.A Kibwezi. Tunafuraha sana tukiwahost leo na mkiwa wageni wetu. Unajua ya kwamba jukumu lile tunafanya ni msaada mkubwa wa taifa letu. Kwa hivyo karibuni nyote kabisa na tuombe.

Baba Mwenyezi Mungu mwenye rehema, ambaye ulianza sheria za ulimwengu, tunakuita asubuhi hii njema, hasa tukinyenyekea sana na tukitubu dhambi zetu mblele zako. Tukijua ya kwamba Bwana sisi hatustahili mblele zako, bali kwa msaada na nehema yako Mungu, utaweza kusikia maombi yetu. Kikao hiki Bwana, tunataka kujiweka mbele zako, wakati huu wakufungua na

kujadiliana, na kuongea mambo ya katiba yetu. Mwenyezi Mungu Baba wetu wa Binguni, tunaomba ukatuongoze, katika kila hatua, katika kila unenaji, katika kila jambo ambalo tutaliongea Mungu, likaweze kuwa na masaada wa taifa ili letu Kenya, wala si msaada wa mtu mmoja, bali kwa wote ambao wanaishi, nakutukuza jina lako, hapa ulimwenguni. Tusaidia siku hii ya leo, wala ukawatawale mawazo ya wale wote wataongoza kipindi hiki, ukatawale mawazo ya wote ambao wataongea, ukatawale mawazo ya wendeshaji wa shughuli hizi zote, ili Mungu tukaweze kubarikiwa na kubarikisha taifa ili letu. Tungetaka kukabidi wale wote ambao bwana wanakuja, wako safarini, Bwana ukawape safari yenye neema, ukawafikishe salama ile Bwana zote tukashikanishwe zote pamoja, katika neema na upendo wako Bwana. Hasa Mungu kuwa nasi kutoka mwanzo mpka mwisho, tunaomba hayo tukiamini Bwana, wewe ndiwe utatusaidia sana sana katika kutengeneza katiba yetu ya Kenya. Katika jina la Baba na la Mwana, na la Roho Mtakatifu tumeomba. Amen.

**Speaker:** Kwanza commissioners mkitukubalia, ningetaka kuwajulisha kwa three Cs wale ambao wamefika leo. Na leo tuko na mkalimani mpya, si ule wa jana. Maanake tunabadilisha badilisha. Kwa hivyo the three C's wale ambao walifika leo, hebu simameni muonekane, tuwatambue. Hawa tulikuwa nao jana, ni Bw. Richard Mhindi, ambaye anatoka sehemu hii, na Christine Mteti, pia anatoka sehemu hii. Hao ndio wamefika lakini kuna mwingine ametoka inje. Bw. Mulei George, ndio atakuwa Mkalimani wa leo, kwa kikao hiki chetu.

Basi, wale ambao mmeudhuria, ketini pahali popote, wale ambao mmeudhuria kikao cha leo, na wakaribisha nyote kwa P.C.E.A. Kibwezi, na kwa kutoa maoni, mbele ya macommissioners. Tukianza na Bi. Mwaimuna, huyo ndio Programme Officer, ndiye anaangalia hiyo mambo ile yatendeke vizuri. Na tuna Secretaries, huyu ndio Mkuza sauti, hata chombo chake tayari ameshatengeneza, na yule ni msaidizi. Tukija upande huu ni Prof. Kabira, tulikuwa naye, mkikumbuka, tulikuwa hapa naye. Mmekumbuka? Prof. Kabira. Na Vice-chairman ama Vice Chairperson, wa Constitution of Kenya Review Commission, yaani hii team ya kurekebisha katiba, ni Bi. Abida-Ali, ndiye Vice Chair Person. Kwa hivyo kutoka hapo, nawapatia programme, ile waendelehe.

**Com. Abida Ali:** Habari zenu, tungependa kuwakaribisha tena, baada ya kukaribishwa na Chairman, katika hiki kikao cha pili, katika hii sehemu ya uwakilishi bungeni. Na, kwa sababu, leo si siku yetu ya kuzungumza ni yenu, tungetaka kuanza na shughuli za siku ya leo. Kwa watu ambao wana memorandums, tutawapatia dakika tano, kusummarise, ama kueleza kwa kifupi, kwa sababu baadaye tutapata nafasi ya kusoma memorandum, hizo ambazo mtatupatia. Watu ambao wanataka kuzungumza, kwa sababu tungependa kusikiliza watu wote watakaofika leo, tutawapa dakika kumi, kuzungumza na baaada ya kuzungumza, kuna register yetu pale, kila atakayezungumza anatakiwa, ingawa mmeandika hapa, kuna wengine pengine wako hapa na hawana maoni. Kwa hivyo tuna register ambayo mtakwenda pale, kujiandikisha na kuna mambo ambayo muhimu tungetaka, kwa sababu ni record rasmi, na watu ambao wana nakala zao, watampatia mwenzetu yule yuko pale, ili tuweze kupata nafasi ya kusoma, wakati mwingine. Tutatumia forms ambazo mmejaza pale inje, kulingana na vile ambavyo mmefika, kwa sababu hatutaki mtu atakayechelewa, kupata nafasi ya kuzungumza mbele yenu, ambao mmefika mapema, ingawa wakati mwingine, itatubidi pengine, tukiona wazee wamezidi na akina mama wamechelewa kwa sababu ya mashughuli nyingi nyumbani,

pengine itatubidi tuwasaidie, ile warudi kuwapikia, mkifika nyumbani mkute kuna chakula. Tutafanya affirmative action. Sawa?

Kwa sababu naona akina mama mpaka warudi nyumbani mapema, nyinyi mkikaa hata mpaka saa kumi, hakuna neno, si ukweli? Asante.

Basi kwa kuanzia, na ikiwa kuna mtu yeyote ambaye ana shida ya kufika mpaka hapa, kwenye microphone ataeleza, tumpelekee microphone mpaka pale ameketi, akiwa kuna mtu aelewi Kiswahi, tuna mwenzetu pale amekubali kuwa translator, nasikia anaelewea Kizungu sana, kwa hivyo atatutafsiria kwa Kizungu ama Kiswahili, kwa sababu sisi ataelewi sana Kikamba. Tusije tukakosea, tunasikia juu juu, kwa hivyo atatusaidia ili tuweze kuwasiliana. Kwa hivyo tutaanza na Bw. Peter Ndambuki. Peter Ndambuki tutakupatia datika tano kusummarise.

**Peter Ndambuki:** Thank you very much. My presentation is in English, so I don't know whether this is acceptable. My presentation is in English.

**Com. Abida Ali:** Go ahead, unaongea na lugha yoyote ile unapenda.

**Peter Ndambuki:** Madam Commissioner, ladies and gentlemen, I am speaking on behalf of the disabled persons of Makindu division. In recognition of the fact that the disabled people are a vulnerable group, we recommend in the new constitution to address the following issues, which pertain to disabled people in Kenya.

1. The issues are accessibility
2. Another issue is communication
3. Education
4. Representation
5. The rights of the individual
6. Employment

I would like to now elaborate on these issues.

The first one accessibility; we would like to see all public service vehicles, with climbing rumps (?) during national conventions or assemblies, and space provided for parking, the assistive devices like wheelchairs.

We would also like to see that roads have, like we have pavements for pedestrians, we would also like to have space provided in our roads to cater for the wheelchairs and arms put on such roads.

We would also like to see, now I am talking about education. If a child has learning difficulties, we would like to see that he is given free and compulsory education and he should be taught by competent and skilled teachers.

On employment; we would like the constitution to address the issue that the employers in the private and government sector to reserve at least 5% of all the jobs available to disabled people.

On the rights; we would like the abortion to remain illegal, because if a lady discovers that the foetus she is carrying is of a disabled child, she can commit abortion. So, we would like abortion to remain illegal.

On representation; we would like each Province to have at least a disabled person in parliament. In local government representation, we would like at least 5% of all local government seats to be reserved for disabled people. Still on the rights; I have talked about abortion and I am now talking about the currency, the Kenya currency. We would like it to have special marks, so that people who are visually handicapped can identify these coins. I think that is all what I have, and now I have a memorandum here.

**Com. Abida Ali:** Asante sana. Paul Kitonga? Tutakupa dakika kumi.

**Paul Kitonga:** Asante sana, commissioners, mabibi na mabwana. Mimi

Ningependa kusema, uraia wa Kenya, hasa kwa maoni yangu yangu nitaanzia na uraia wa Kenya. ningeonona yule angekuwa mkenya kamili, awe ni yule babu wa babu yake, yaani mababu wake wamezaliwa hapa Kenya. Hasa kuanzia wakati ule wa ukoloni, na ile mipaka iliwekwa. Huyu wazazi wake waliokuwa hapa, huyo ndio kwa maoni yangu naona anafaa ahesabiwa, ndio mkenya hasili, kwa uwandikishaji wa wakenya.

Ukenya wa pili, au mtu kuwa mkenya pili; kuna wale wanaokuja, kwa maoni yangu naona mtu akija kama mgeni katika Kenya, akae kama miaka karibu tano, akiangaliwa hali yake, na pawekwe masharti kulingana na sheria zetu za Kenya, zile anafaa atimize ndio awe mwanainchi wa Kenya. Lakini, awe, yale anayofanyiwa mwanainchi wa Kenya kwa kuzaliwa, mengine kama mali hasili, awe awezi kuhusishwa. Lakini sheria za Kenya, awe anafuata ipasavyo. Akivunja sheria, atahukumiwa kama mwana Kenya wa kawaida, yule amezaliwa hapa, kutoka mababu. Huu nimeongea ni uraia.

Pili, ningeeongea katika haki za mwanainchi wa Kenya na kazi zao; kwa maoni yangu naona, mkenya ana haki katika mali zetu za haki. Kama, mchanga au land kwa lugha ingine. Tuwe tunagawiwa mashamba. Kama mwanaume anapata heka ishirini, mwanamke naye awe anapata heka ishirini, zote katika Kenya. Na, hiyo mashamba, maana inchi yetu ni kubwa, inaweka katika katiba hii tunayotengeneza mpya, ikatafutiwa namna kwa wale wataalamu, ikawa kila mtu anaweza kupata shamba. Hiyo ni haki moja ya mwanainchi wa Kenya, kwa maoni yangu naona, anafaa apate, mkenya yeyote.

Haki ya pili, naona kwa mkenya kupatiwa haki ya kama maji masafi ya kunywa na kufanya mambo yote ya nyumbani, na ikiwezekana, kama pesa zitakuwepo, na zitakuwepo kama serikali itakuwepo nzuri, kulingana na katiba tunayotengeneza,

ambayo itakuwa ni ya mambo yote yafanywe sawa, kulingana na sheria zilioko. Awe anawesa kupower hata maji ya kunyunyizia mashamba, tuwe na chakula cha kutosha. Kila mtu awe asumbuki.

Katika haki za kikazi; kwa maoni yangu ningeona kila mkenya, wale wako na umri wa kufanya kazi, kuanzia miaka kumi na nane kuenda juu. Awe akipatiwa kazi moja, na akifanya akifika miaka hamsini anatoka kazi, ana retire, anaingia mwingine. Na mtu mmoja awe na kazi moja, kama ni mfanyi biashara, ni mfanyi biashara, kama ni mwalimu ni mwalimu, na hana tukazi twingine twake twa pembeni. Hiyo ni maoni yangu. Naona kila mkenya awe na kazi moja.

Ile ingine ni mambo ya matibabu; Kwa maoni yangu ningeona, kila sub location, pawe na ata kama ni health centre, na pawe na dawa za kutosha, na daktari ata at least ni clinical officer, qualified, anayelipwa na serikali. Na dawa ziwe za bure, ziko za kutosha na kama kuna mmoja atapotoka, kama ni daktari, ashtakiwe kulingana na sheria zilioko. Lakini, mwanainchi apate dawa bure, maana ni kodi ikisimamiwa uzuri kulingana na sheria, itakuwa tunalipa, na tunalipa hata hivi sasa, kodi ya kutosha, ya kununuliwa madawa, tukanywa bure.

Kile kingine ni elimu; elimu kwa maoni yangu, naona watoto wangesoma kwa fees kiasi, ya primary education, lakini majengo yawe yanajengwa na serikali na kodi yetu, ile tunao toa. Na kamati ya shule iwe inasimamia hiyo shule, na vifaa vyote vya shule visiachiwe mzazi, viwekwe na serikali, kwa kodi yetu ile tunatota. Vitabu vyote, ata ruler, ata geometrical set. Kila kitu, kwanzia standard one, mapaka standard seven au eight, itakavyo kuwa, na mwalimu alipwe na serikali kwa kodi yetu. Na kutoka hapo, ningeomba kulingana na vile itakavyo kuwa, maana naona tutaweka katiba mzuri. Elimu iwe ya bure kuanzia secondary school mpaka universities, mtu agraduate, na aje atumikie inchi hii.

Nafikiri nimeongea mambo ya mchanga, sasa nitaongea mambo ya uwongozi; Bunge, mimi naonelea katika bunge yetu, iwe kama inavyo kuwa na constituencies zilioka, maana naona tuna wajumbe, kulingana ninavyo fahamu, mia mbili na kumi. Pawe na wanawake, wale watakao kuwa nominated, ata wakiwa nusu, wale nominated na wakipigiwa kura, wakipita pia si neno, maana ni viongozi. Lakini wawe wanakuwa nominated, wanawake wakutosha, katika vyama hata mbalimbali, ata kama ni kimoja, lakini wanawake wawepo number ya kutosha kuwakilisha wanawake. Kwa hivyo, wabunge wawe, kama vile walivyo sasa.

Lakini, mtu kuchaguliwa mbunge, kwa maoni yangu naona, yeye angekuwe ni mtu ameeelimika, maana kuwakilisha watu, mpaka uwe ni mtu ana ufahamu mzuri katika mambo yaliyoko, katika siku hizi. Awe ni mtu at least ako na university education, na awe kidogo ana fahamu sheria, sio awe constitutional lawyer lakini at least, awe ana fahamu mambo ya sheria, na awe ni mtu wa university level.

Kama ni president; ningeomba huyo awe ni mtu constitutionally ako sawa, yaani katiba ana ifahamu kuanzia mwanzo mpaka mwisho na awe ni mtu wa kiwango hicho cha university. Na awe na umri ule ule unaokuwa, naona sio mbaya, wa miaka

thelathini na tano, lakini awe ni mtu wa elimu ya university.

Nitakuja kwa hawa wakitoka katiza kazi zao, kama president. Awe akipower kiasi fulani cha pension na akae kama raia wale wengine. Hakuna malindikizo ati ma security na nini, kwani aliuwa. Akae tu kama mwanainchi wa kawaida, lakini kwa kurudishiwa asante, kwa kuwa alifanya kazi mzuri, ata kama ilikuwa mbaya. Akishamaliza wakati wake wa miaka kumi, maana tuna vipindi viwili na ninaona ni vizuri hivyo, akae na kama ni pension ya karobo ama ka third, whatever it is, ya ile mshahara alikuwa akipata, atosheke na hako, maana katika account yake, nafikiri apakosi kitu. Na Members of Parliament, wawe wakifanyiwa ivyo ivyo. Kwa hivyo, kwa maoni yangu, sioni hapo pakiwa pazuri, mtu akilundikiwa kila kitu awe ni yeye.

### **Councilors. (Interruption)**

**Com. Abida Ali:** Mzee fupisha saa yako imeisha, fupisha tafadhali.

**Paul Kitonga:** Asante. Councilors wawe ni watu wa secondary level, na awe ni mtu anaweza kujielesha kwa lugha vizuri na walipwe kisawasawa.

Administrationwise, au kimkoa au vile tunavyosimamiwa kimkoa. Ningeomba badala ya kuchukuliwa mtu na watu, au na mtu mmoja, tuwe kama P.C anakuwa governor na anakuwa elected na watu. Na D.C, na D.O, na Chief, na Sub-chief waondolewe, sioni wana aja. Na awekwe mzee wa kijiji na awe akilipwa, hiyo ndio administration. Naona katika appointments, pasiwekwe mtu mmoja, kama president anavyofanya siku hizi. Iwe kama ni Chief Justice, awe appointed in the parliament, kama ni ma commissioners, wawe wanachukuliwa na let's say, members of parliament, ambao wao wamepower within au mandate na sisi wanainchi. Wawe ni commissioners wamewekwa, kama ni Electoral Commissioners, hao wakutufanyia mambo ya uchaguzi, au ni commissioner ata kama hawa sasa, wanatufanyia mambo ya katiba, na mwingine yeyote asiwe appointed awe mtu wa mtu. Awe ni mtu wetu ako na idhini. Na hata mbunge, ningeomba, kama amekosea katika kile kipindi cha miaka tano, asiachwe, atafutiwe namna ya kuondolewa na wanainchi, awekwe mwingine, maana ataturibia wakati. Ni hayo tu, asanteni.

**Com. Abida Ali:** Asante sana mzee. Kanini Ngumbi? Kanini Ngumbi dakika tano, kwa sababu una memorandum.

### **Kanini Ngumbi:**

**Translator:** Nashukuru kwa kukatibishwa kunena hapa. Ninashukuru kwa wageni wetu ambao wamefika hapa. Nashukuru wamekuja na vitu vimetengenezwa na mikono na hawajaumia.

Nitaanza kunena maoni, ambaye ni single mothers. Maoni tumeona moja ni tusomeshe watoto wetu.

Ya pili ni kutafutiwa mashamba.

Ya tatu ni kutafutiwa pesa, ambayo tunaweza kuanza small businesses. Asante.

**Com. Abida Ali:** Asante sana, tumeambiwa mheshimiwa amefika, sijui kama nimeona akitoka ama yuko ndani? Haya, mheshimiwa would you like to say something.

**Mheshimiwa:** Thank you all commissioners. Since I gave my views yesterday. I want to add a little.

As I said yesterday, on presidential election; he must have one constituency called Kenya. He should not be a member of a constituency, as that will upgrade his responsibilities. He would have a shared responsibility as a Member of Parliament and the president of the country. That president when elected, the current constitution gives him, only 25% votes for five Provinces. We should wish to have a president who has a command majority and he should with the votes casted, he should not attain less than 51% of the total votes. His running mate, would be assured to be the Vice president for the entire period. Members of his cabinet, should not come from the Members of Parliament elected. We should have people who have no other responsibilities to run this government, and let the responsibilities of Members of Parliament be their constituencies only.

Those members of cabinet, who shall be appointed, let them be vetted by the National Assembly. To see their records, their performance and ability to perform. Equally the Attorney General and all judges of High Court, to be vetted by parliament.

On land issues; this issue of land, any land, which is in existence, now, is formation of this constituency, shall any land belong to the government and where people are living now, shall no longer be a Crown land or State land. It will be entrusted to the people who live on it without any other condition. Because, the constitution we have, gave protection to those people who used to own land before our independence. That was May 1963, only those people who were living on their own land, were given Titles, but those who acquired land after independence were not given Titles and became squatters on their own land. This is something, which must be revoked by this constitution we are now making.

People living alongside, National Parks, or conservation areas of the wildlife; the County Council, who are occupying the National Parks, should be given the full mandate of running the National Parks, within their area of jurisdiction. This question of a body running from Nairobi, and the people who are living near the Parks, when their crops are destroyed, nobody cares about their compensation, should be abolished, let the County Council run the National Parks. Let the people who live in the National Parks be compensated fully for any food destroyed by the animals, let the people who are maimed on or killed by the wildlife, let the compensation not be less than 3 million per person. And, this is what parliament has agreed. Therefore, let this new constitution, because the government has been unwilling to bring the Bill, now let this constitution review put that



recommendation, any compensation must not be less than 3 million, there is no limit.

On issue of land; as I said, let the natural wealth, on any portion of land owned by a Kenyan, if there is gold, diamond, oil on that part of land, let it be so owned by the owner of that portion of land. The question of somebody coming and claiming to own that area which is his, should not arise, let the land be owned by the person, and the natural wealth within be owned by the same person.

As I said on the issue of Provincial Administration; this is an office issue be scrapped. This was a tool of the colonial government to suppress Africans, and not that we are free people, and we have got an elective procedure, the question of Chiefs, Assistant Chiefs, D.Os, D.Cs and the P.Cs should be abolished. It is because; there is a conflict of interest because when I am elected a Member of Parliament for Kibwezi, I have got other people running side by side, called District Officers, and they try to come and give a wrong image to the elected people who have the mandate of the people in that constituency. Therefore, the question of D.Os, Chiefs should be done away with, and if it is the wish of the people of Kenya, and we may want to have the Province retained that, that man to head the Province should be an elected person by the people of that Province.

Commissioners; On the education, this is mandatory and this is a big part of the government. It should be given for free, we are paying a lot of taxes, and I said yesterday, Kenyans are tired of Harambee business, every year, Harambee Harambee. We are paying taxes and we are again paying direct taxes to the Dual development. It is either the two. Let the government remove the taxes of V.A.T Income Tax all together, and let people do their own constructions of schools and dispensaries, or we stop Harambees and we pay taxes. It is paid to ceasar what belongs to ceasar and to God what belongs to God. So, we have been paying our dues to the government and the same government, when we want to put up a primary school, you construct a primary school, you put up the furniture, you put up the books and whatever. And to date we are now paying the teachers, what about the government. So, if they cannot account for our taxes, then mwanainchi should not be taxed again on Harambee business.

People with disabilities; people with disabilities should be looked upon, those people must be given specialized training and in parliament there must be a portion, a percentage for the people with disabilities to occupy, some percentage of seats, in the National Assembly. And since most of my things, I talked yesterday, I just wanted to tell the people we give our proposals, because this is the only chance, you and me, your chance to say what you want in the constitution, because if you don't do it, you have nobody to blame and I tell you what we say here is what the parliament will pass. There will be referendum to agree on this. Thank you.

**Com. Abida Ali:** Asante sana mheshimiwa, Wayua Peter, Wayua Peter, hauna maoni? Okay, Jackson Kavenya? It is okay we will bring the microphone there, it is okay.

**Jackson Kavenya:** Sina maoni, isipokuwa ni machache tu. Sisi watu kama mimi walemavu, shida yetu ambayo tunapata, ni kusafiri mahali, tunapata taabu sana, sababu hakuna kitu ya kusafiria, tunaona watu wanaenda, wakikuja. Basi, sasa tukiwauliza mliona nini? Hawatuelezi sawasaw, kama serikali yetu ikiwa inaweza kutupatia kama vitu vya kutembelea, kama wheelchair, inakuwa sawasawa. Kwa hivyo, hata, hatuwezi kuwa tumesoma sana, sababu shule iko mbali. Na tukienda kwa shule, hata mwalimu, akikuangalia hivi anaona aah, huyu mtu, mlemavu huyu aah, wengine wanatufukuza tu. Kwa hivyo tunataka serikali iwe inatuangalia, kwa sababu, walemavu, hata serikali ile ambayo iko, tunaona hatujulikani. Sababu ukienda kwa office, unakaa inje, wenzangu wanaingia wanaingia, karani akija akikuona akuambie aah kuja kesho. Sababu hatujui kama, hawajui kama tumetoka mbali. Kwa hivyo, hata tukifika ma office zingine, tunakuta ile vitu ya kuingia ndani, ni juu sana, hauwezi kuingia. Sasa tunataka matajiri wakijenga nyumba, wajenge sawasawa, tuwe tunapita, hata tunaingia kule ndani. Kwa hivyo, hat serikali ambayo inaundwa, tunaomba mlemavu wowote, mwenye miaka kumi na nane, awe anaweza kupatiwa, hata kitu kidogo, sababu tukienda kwa ma hoteli ama nini, tunaona wenzetu wanakula, sina ndururu, sina kazi. Sasa serikali ikinipatia kila mwezi, shilingi ata mia tano, ningeingia na wenzangu tunakula, sababu nina kitu. Lakini kwa sasa, kama ukiwa namna hii, mpaka ukae nyumbani tu, ukae tu, kwa sababu maomb yetu ilikuwa imeandikwa na mwenzangu mimi nilikuwa tu nikuongezea tu, sina mengi ni hayo tu.

**Com. Abida Ali:** Nauliza, kabla haujamaliza, watu wengi hapa tunasikia wakiongea kuhusu serikali, na haki zingine. Baada ya kutuambia vitu zile ungetaka kuona kama mtu ambaye ni mlemavu, kuna mambo mengine ungetaka kuona, katika kwa mfano, serikali, ama mambo ya mashamba, kama wanavyoongea watu wengine?

**Jackson Kavenya:** Eeh sababu, walemavu wahesabiwe, wapatiwe mashamba. Ukiona mlemavu unaona, saa huyu mlemavu apatiwe shamba na hana kitu, awezi kulima, awezi nini. Serikali aipangi mlemavu kama ni mtu wa kupewa shamba. Hata wengine, walemaavu tunakaa vile, hakuna wake, hakuna nini? Sababu wanawake hawakutaki, kwa hivyo sasa, shida ni nyingi sisi. Kwa hivyo, mambo inakuwa kwetu, ni ngumu, serikali ituangalie.

**Com. Abida Ali:** Asante sana, Richard Mhindi, Umesema Political Parties, sijui kama ni chama gani, kwa sababu Political Parties is too general

**Richard Mhindi:** S.D.P

**Com. Abida Ali:** S.D.P Okay.

**Richard Mhindi:** Asante. Nitaanza na utangulizi wa katiba. Katika katiba ilioko sasa, katika utangulizi, mwanainchi wa Kenya hajatajwa kamwe katika katiba, na ningaliomba katika katiba, mwanainchi wa Kenya awe katika utangulizi wa katiba, kwamba sisi wanainchi wa Kenya hiyo ianze katika katiba kama utangulizi.

La pili, ni ukuu wa katiba. Hii katiba ningeliomba, iwe ndio katiba kuu, kushinda katiba zote katika inchi, iwe ndio inasimamia kila kitu, ndio iko juu ya kila kitu.

La tatu ni juu ya uraia. Vile katiba ilioko, vile imesema kwamba mtu ambaye alizaliwa mwaka 63, ndio inaruhusu awe mwanainchi wa Kenya. Kwa hivyo ningelitoa maoni yangu kwamba, yule alizaliwa baadaye ya mwaka 63 na kabla ya mwaka 63, aandikishwe kama raia wa Kenya. Na kama ni msichana, ambaye ameolowe, na mtu kutoka inchi za inje, na wamekaa hapa Kenya na wanaishi hapa, kama baada ya miaka mitano, waandikishwe kama raia wa Kenya. Na kama ni mwanamke wa Kenya, ameolewa inje ya Kenya, na anaishi hapa Kenya, na mwanaume wake ama mme wake, na wameishi kwa miaka mitano, waandikishwe kama raia wa Kenya.

La nne ni juu ya usalama wa taifa. Kuna haya mambo kama tribal clashes, mambo kama kayambombo. Ningeliomba katika katiba yetu, mwanainchi wa Kenya, alindwe vilivyo na katiba, na kusiwe na tashishi ama kuuliwa kwa raia wa Kenya kupitia kwa mambo ya tribal clashes, kwa hivyo usalama wa taifa, uimarishwe.

Vyama vya kisiasa; Ningeliomba ama maoni yangu juu ya katiba, kwamba vyama vya siasa viwe kama institutions ambazo nizakuleta maendeleo katika inchi ya Kenya, sio tu siasa peke yake. Wawe wakifanya mambo kama ya maendeleo ya kujenga mashule, miradi kama ya maji, na vile vilve vyama vya kisiasa vipewe haki, katika mambo yote, kifedha, zipewe pesa na serikali. Katika media, utangazaji, viruhusiwe, viwe vyote vinashiriki katika kila jambo.

Ilo lingine ni juu ya miundo ya serikali; ningelitoa maoni yangu kwamba tuwe na muundo wa serikali ya mseto katika serikali yetu. Tuwe na serikali ya mseto na chama ambacho kimepata viti vingi bungeni, kiunde serikali, lakini vyama vyote vihusishwe katika kuunda serikali.

Lingine, ningelizungumzia juu ya tanzu tatu za serikali. Tanzu ya bunge, tanzu ya raisi na ya sheria. Zitengamane, kila moja iwe, iwe na uhuru wake, kama ni tanzu ya sheria, ijisimimamie vilivyo, bila kuingiliwa na tanzu lingine lolote. Kama ni tanzu la raisi zile nguvu zipunguzwe kwa kuwa ni nyingi sana. Zipunguzwe, raisi asiwe ndio wa kuaajili, ndio wakuvuta, awe na zile nguvu zake, ambazo zinamfaa. Vile vile bunge, ipewe zile nguvu zake, ambazo zinasimamia bunge.

Ile lingine ningelizungumzia ni juu ya serikali za mtaa; serikali za mtaa zipewe uhuru wa kuwaajiri wafanyi kazi wake na ma officer kama clerk town council, awe akiajiriwa na serikali ya mtaa, ikiwa uhuru. Sio atoke katika local government. Vile vile zile pesa ambazo zimetoka katika County Council, zisaidie lile eneo ambalo, ile Municipal, ama ile council inawakilisha, zile pesa zitumike pale, vile vile, County Council ipewe nguvu kama ni Mayors, kama ni chairman wa County Councils, ama Mayors wa Municipals. Ma mayor na wenye viti, wawe wakichaguliwa na wanainchi. Wakichaguliwa na wanainchi, mahali ambapo Mayor amesimama kama ni Makueni, achaguliwe na wanainchi, kama ni chairman wa County Council. Na kama ni maendeleo

ya wilaya, Mayor ama mwenyekiti wa hizo wilaya awe ndio mwenyekiti wa maendeleo.

Ile ingine ni muundo na utaratibu wa uchaguzi. Ningelitoa maoni yangu kwamba, Electoral Commission, iwe independent, iwe free and fair na iwe kama wale commissioners, ishirini na mbili walioko sasa, wapunguzwe. Wawe ni kama commissioners kumi na tano na wasiwe wanatoka kwa vyama vyovyote, wachaguliwe na wabunge, lakini wasichaliwe kulingana na vyama. Vile vile, Electoral Commission ipewe uhuru wa ku prosecute, electoral offenses ikiwa uhuru. Vile vile, upande wa uchaguzi, ingelikuwa maoni yangu kwamba, kuwe na uchaguzi na uraisi, achaguliwe peke yake, kuwe na uchaguzi ya wabunge, wachaguliwe peke yao siku yao, kuwe na uchaguzi wa councilors na chairman wa County Councils ama Mayors wa Municipal ama wa miji nao wachaguliwe siku yao, ndio kuwe na nafasi ya uchaguzi.

Vile vile ingekuwa ma qualifications za uchaguzi. Mtu kama amesimama uraisi, awe ingekuwa pendekezo langu, awe ni mtu wa degree level, na awe ametoka kwenye chuo ambacho kinatambulika. Kama ni mbunge, awe ni wa form 4 na kuenda juu, na awe amefuzu ama amepita vizuri katika mtihani. Kama ni raisi awe mwanainchi wa Kenya, awe ameowa ama ameolewa, awe na akili timamu, awe amejieleza kama pengine alipata mali kwa njia ambayo haifai, ajieleze vile alipat mali yake, ndio aweze kukubaliwa kuwa raisi wa inchi. Vile vile, raisi awe ni mtu ambaye agombe kiti cha ubunge.

La mwisho, ni juu ya haki za kimsingi. Basic rights; kila mwanainchi wa Kenya, ingekuwa maoni yangu, apewe haki ya elimu, haki ya matibabu, haki ya mashamba, haki ya maji, apewe na serikali. Lakini, katika hizo haki, kuna moja ningeliomba ichunguzwe, haki ya kuabudu. Imekuwa na tashwishi sana. Haki ya kuabudu, ningaliomba iletwe huku chine, locational level, ndio kama ni kanisa inajengwa, viongozi wa locational level, wawe na kamati ya kuchunguza ile kanisa ambayo inajengwa ni kanisa aina gani? Hapo ningaliomba hiyo haki ya kuabudu ichunguzwe na viongozi kutoka locational level.

Ile ingine ningeliongezea ni juu ya makundi madogo madogo kama ya akina mama, kama akina vijana, walemavu, kabila ndogo ndogo, kama watu wa North Eastern, haki zao ziangaliwe, wahusishwe katika kila ktu, kama ni bungeni, kama ni administration, kama ni maendeleo ya kijiji, wahusishwe katika kila jambo.

Nikiongezea vile mwenzangu, mlemavu hapa amesema, kama ni manyumba ijengwe, mlemavu akikumbukwa, kuwe na mahali pa kupitia zile gari zao. Kama ni bus iundwe ikiwa kuna nafasi yao ya kuweka gari zao ama kuingia kwa njia inayofaa. Kama ni simu, unakuta wana shida ya simu. Wawe na call box fupi, ambazo wanaweza kupiga simu kama wale wanainchi wengine wote wale.

Kama ni akina mama, wahusishwe katika maendeleo ya inchi, katika kugombea kila kiti, kulingana na zile qualification zao, ama kwa njia nyingine ningelisema, katika katiba, tuwe na affirmative action. Ndio wote wahusishwe.

Lile la mwisho commissioners, ni juu ya ardhi na mali; ningeliomba ama maoni yangu kwamba, katika katiba hii, hili jambo la

ardhi liangaliwe vilivyo na kama ingeliwezekana, kila mwanainchi wa Kenya, awe na ardhi. Na vile vile ningeliomba, mipaka ya inchi hii iangaliwe vizuri, ndio kila mtu ama kila kabila, kulingana na ule mpaka, ambao uliwekwa na mkoloni, mwaka 1934, uangaliwe vilivyo ndio kila kabila ama kila mtu a retain, ama kila kabila iwe na ule mpaka wake wa kawaida, kulingana na katiba ambayo iliwekwa mwaka 1934, juu ya ardhi. Vile vile, upande wa ardhi, ningeliomba, kila mwanainchi apate Title Deed, akipewa ardhi.

La mwisho commissioners, ningeliomba haki za kitamaduni ama customary law. Kama ni customary law ya wakamba, kuna mambo kama ya 'ndeo; kuna kitu inaitwa 'ndeo' kuna kitu inaitwa 'mbanga', kuna kitu inaitwa 'kithio', hivyo zihusishwe, vya kabila kama ni ya wakamba, vihusishwe katika katiba, kwa kuwa ile mila, waswahili wanasema 'Mwacha mila ni mtumwa' ile mila yetu ya wakamba iuzishwe vilivyo katika katiba, kulingana na vile mila za wakamba huwa ziko.

La mwisho ambalo ningemaliza nalo, ni juu ya transfer of powers and succession. Kama ni raisi anatoka, amemaliza vipindi vyake kama ni viwili, ningeliomba tu kama raia mwingine yeyote yule, sio kusema kwamba apewe askari, apewe magari, apewe ma allowance makubwa, na yeye amefanya kazi kama wafanyi kazi wale wengine wote ambao wana retire baada ya miaka 55. Aende nyumbani vilivyo, akapumzike, na kama ni kupewa, ile allowance, kama mfanyi kazi ule mwingine yeyote, apewe hivyo hivyo, lakini sio apewe tofauti na wale wafanyi kazi wengine. Kwa hayo machache, asanteni.

**Com. Abida Ali:** Asante sana, na tunaambiwa kwamba D.O wa upande huu amefika, tungependa kukukaribisha, na Bwana D.O tunashukuru na pengine ukiwa na maoni, utatujulisha tukupatie nafasi. Ama unataka kusema chochote kwa wakati huu pengine. Asante. Mary Mwangangi?

**Mary Mwangangi:**

**Translator:** Nashukuru kwa kukaribishwa na kukubaliwa kuja kunene hapa. Sina maneno mengi isipokuwa, kile kimetufikisha kwenye mkutano huu ambayo ni mhimu sana ni kwa sababu tunaishi kwa masquatter. Kwas sababu sisi tunaishi kama masquatters. Tunauliza tutafutiwe pahali ya kuishi. Sisi ni masquatter upande wa Masonga, tunalima huku na tunalala pahali pengine, kwa sababu hatuna shamba. Nauliza wale wasichana ambao ni single mothers na wamezalia kwao, wale watoto ambao wamezaa, kuna wengine wamezaa watoto na walikuwa single mothers na wamewacha wale watoto na grand mothers wao, na wao wamekufa, na wazazi wao hawana nguvu. Tunauliza watoto hawa wasomeshwe free na pia watafutiwe pahali pa ku settle.

Sisi tunaviwete nyumbani na hatujajua wanapelekwa wapi kwa masomo na msaada mwingine. Tunauliza wale wanachukua haya majina, wakuje kwetu tuwapae haya majina ili hawa viwete wapate msaada. Asante mimi nafika hapo sina mengine.

**Com. Abida Ali:** Asante mama. John Nguno? We will give you five minutes, since you have a document that we undertake to read.

**John Nguno:** Thank you commissioners. Nachukua fursa hii kwanza nitoe shukrani kwa nafasi hii, niweze kuongea, kutaja ka uchache kwa niaba ya wenzangu retirees, yaani walio staafu ambao walikuwa katika serikali yetu.

La kwanza, ningependa nitaje, retirees wawe wakifikiriwa nyogeza ya kila mwezi. Kwa sababu wakati walikuwa wakifanya kazi kila mwaka, walikuwa wakipata percentage ya nyongeza.

La pili, ningependa serikali yetu, iwe ikifikiria kutuma ma officers, waje ktika constituencies na kufanya mikutano na wale waliostaafu, kuwapa motisha, kuongea na wao, kwa sababu wao ndio wamejenga inchi hadi kiwango kinachoonekana sasa.

La tatu, kuwe wakati wa mikutano, ambayo itapangwa na serikali, wawe hawa retirees au wastaafu wakipatiwa zawadi, encouragement, wawe wakiwa encouraged, wapatiwe ata kama ni taa, kama ni jembe au ni torch, waambiwe waendeleo, kwa sababu wengi wao, wengi wa hawa, wana hata sasa wanafanya kazi hata wakiwa wako nyumbani, wana ujuzi wa kusaidia inchi yetu kuendelea.

La nne, ile mishahara, zile pensions, cheques, zitumwe mapema, kutokea tarehe ishirini na tano zitumwe kwa banks au kwa post banks, ile waliostaafu wawache kunungunika hapa na pale. Ikitumwa kutokea tarehe ishirini na tano, kufika tarehe moja , tarehe mbili, mtu atakuwa amejua atafanya nini na zile pesa. Hiyo tunaona wakicheleweshwa na hiyo, ni jambo naomba iwe reported.

La mwisho kuhusu ile memorandum, ni wakati waliostaafu wako katika public forums, kama mikutano, ni ya D.C, ni ya D.O, ni ya Chief, wawe recognized, hata wakati programme imepangwa , kama ni D.O ama ni Chief, aseme yule officer aliyeretire pale asalimie watu, kwa sababu hii inampa awali kuonekana wako, si ati walikwisha.

Ninaomba kupitia kwa ma commissioners, kwa sababu zile points nilikuwa nazo nimemaliza lakini dakika zangu zingali ziko, ni zungumzie kuhusu Education Act kidogo, asante kwa kuniruhusu. Nataka kuzungumza kuhusu education Act Cap 211 ambayo sasa ndio inshughulikia elimu katika inchi yetu ya Kenya. Ninaomba wazazi, sana sana katika secondary schools, wapewe wajibu mkubwa ku manage shule zao, secondary school zao. Kwa sheria ya sasa, ambayo ina govern education, hawana uwezo, uwezo ule huko pale, umepewa sana ni mwalimu mkuu, headmaster, ndio executive officer. Akikohoa anakohoa, hata akitaka kusukuma shule ikaanguke watu wananyamaza pale.

Ninaomba pia, sababu wazazi wamepewe nafasi yao kama wenye kuunda ile shule ninaomba ma D.E.Os wawe wameelimika kiwango ca degree older, na pia sababu ana simamia shule nyingi pale, secondary na pia anasimamia primary schools, awe ana degree.

District Educational officers, awe ana masters degree, nita elaborate hapo. Master's degree in education. Na District Education Officer, awe ana uwezo, kupitia kwa education Act, ile itakwenda kutengenezwa. Yeh, kukoowa katika district, akinena mambo yote kuhusu elimu, akisikilizwa, na secondary school headmastes na wote na walimu wa primary wamusikize. Akiwa akufikia hiki kiwango cha masters, awezi kuongoza wwalimu wa secondary, kwa sababu wale tuko na wao, wamefikia kiwango cah kuwa D.O on merit. Shauri amefanya kazi siku nyingi. Na akitaka kuongea, akinene, akihutubia wale wa ma principals wa secondary schools, hawamsikizi, wanasema, he is not educated. Na tuko na shida hii, Kenya mzima. Wawe wamepewa mamlaka yote ku control primary and secondary schools.

**Com. Abida Ali:** Asante mzee, time yako imekwisha, pengine u summarise:

**John Nguno:** Ma P.Ds wawe ni Education Cordnators katika Province. Mambo yote yaenda diret katika Jogoo House, lakini ipitie kule kama formality. Ndio apewe uwezo wakumaliza kila kitu, kuhusu mashule yake.

Ile ya mwisho ni kuhusu, secondary schools heads conferences. Si amemaliza kazi, hizo zikwishe, zirudishwe katika district. Kenya mzima wakati wa mwezi wa June, ma principals wote wanaenda kukutanyika mahali fulani, na wanabeba ma pesa ya shule ya wazizi wanaenda kukanyagia hulo. Unaona shule mtu anaondoka na elfu hamsini, anaenda, akirudi anatengeneza cash payment voucher, hiyo amemaliza huko. Hiyo hatutaki, kabisa hatutaki. Kama ni mikutano hiyo, ifanyike katika district levels, na kuwe pinpointed, viongozi wenye ujuzi, kuenda kukaa na wao, ili tujue wanapanga nini, kwa sababu wanatumia pesa zetu. Na zile pesa wanachukua kuenda kutumia huko, ziwe zimekuwa authorized by B.O.G members, sio kubeba tu, mtu anachukuwa one hundred thousands, anarudisha elfu ishirini. Hiyo inaendelea na katiba yetu itutengenezee mipango kamili kuchunguza, kwa sababu wanainchi wanamalizwa kabisa. Thank you very much for listening to me.

**Com. Abida Ali:** Asante sana. Ruth Mativo, dakika tano tafadhali Ruth.

**Ruth Mativo:** Thank you commissioner. Niko hapa nasimamia wanawake, wale widows. Ama wale mabwana zao wamekufa.

Maoni yetu ni kwamba serikali kitu ya kwanza, hawa wanawake wakiwachwa na ma bwana zao, kuna watoto wao, hawawezi kusoma. Twaomba serikali iangalie masoma ya watoto hao.

Kile kingine, tungeomba kuna wanawake wengine wanawachwa wakiwa wadogo sana, wakiwa na watoto wawili, mtoto mmoja, na wako na uwezo wa kufanya kazi. Pia serikali iangalie hao wanawake wanaweza kufanya kazi ama wako na elimu, watafutwe ma kazi ili wasaadie watoto wao.

Inginge ya tatu ni, kuna wengine wanawachwa bila makao. Pia serikali iangalie, kukiwa na ardhi mahali, wapewe makao, na

kukaa na watoto wao.

Ya nne, ningeomba serikali, kuwe na shirika ya wanawake wale wamewachwa na mabwana zao Kenya. Watambulike, ile wajisikie kama wako na wale wengine.

Ile ingine, wakati wa shule, kuna bursaries zinatumiwa huko kwa mashule, na badala watoto wa wale wanawake kuptiwa bursaries, zinapatiwa watoto wale waarefu sana. Na ule mtoto wa ule mmama anakosa fees. Ningeomba serikali iyangalie bursaries kwa hao watoto.

Ile ingine, ningeomba serikali iyangalie, kuna ma kazi ndogo ndogo kama ni ya council, ile ya uko katika health centres, dispensaries. Wanawake hao waingizwe huku, ikwa ni kufagia, wapate mkate wa kila siku. Asante.

**Com. Abida Ali:** Asante sana, Nicodemus Mativo, mbona majina yamefanana?

**Nicodemus Mativo:** No relations at all. Commissioners, ladies and gentlemen. Mine is very straightforward.

One, I will touch on the national resourced.

- (i) Land : In this constituency we have tracts of land this area. Another piece has been extended to university, while you have heard here a lady, saying that they are living as squatters. People were moved from Chulu, settled there with nothing else. Only to be dumped there, construct whatever you can, but still the land is there. It is within here, the same. So land, the question of land, we want a good arithmetic, that is each citizen to have about one to five acres, any other idle land, tax it and we would get a lot of money and that will create finance. With this finance, which of course is one of our resources, we need it to be controlled, we need the finance minister, and we need the auditor general, financial controller to be in charge of the national finance. And by appointing these persons, the parliament should also have power to endorse them, to say yes you are qualified for that job, because it is controlling one of the important national resources.
- (ii) Human resources; at the age of 18 years, each one is given an I.D card. Well, the government should also know that from there, they have certain numbers of Kenyan citizens to look after, to cater for education and also to pay monthly allowance. Why not increase the N.S.SF, why not to move abroad, at least so that N.S.S.F can also pay a person who reaches the age of 21 years.

On succession; yes, after an election, it is good to have all the votes counted at the polling station. This is beat up the results. The president if to be elected, has to be elected by about 60% or over 61% per cent. However comes next becomes an automatic Vice president. After all Kenyan citizens have already taken part in election.



For the M.Ps, with education; minimum form 4, and if the people in the constituency want to recall their M.P, ten thousand people should sign the memorandum to remove him.

On the councilors; education should be O'level, and if the people in that ward want to remove him, well only 2,000 people should sign the memorandum to remove him. So that to create balances. So that no one will sit there doing idle things.

The next one on succession, when there is election of the presidency, then the Attorney General, should take over the office, that period, and then from there, if he is elected within the month, he is sworn by the Chief Justice, and that will mark a new. And then the handing over is done within one month.

On another point of issue, about the H.I.V victims, it is a dangerous disease and it has taken many of the Kenyan citizens. So, those who have been left behind, as a result of such, I think they be given assistance by the government. And with that one, I end up my memorandum.

**Com. Abida Ali:** Now please ngojea mzee kidogo, we want a clarification.

**Speaker:** Mzee Nicodemus, umesema wale wamefika miaka ishirini na moja, wapatiwe pesa na N.S.S.F. Ni kila mtu at wale wameandikwa na wale wajaandikwa

**Nicodemus Mativo:** Hata wale ameandikwa ama hajaandikwa. Yote iwe ni mamoja

**Speaker:** So you are proposing a welfare society.

**Nicodemus Mativo:** That is the way it is.

**Speaker:** Okay thank you.

**Com. Abida Ali:** Asante Professor. Elizabeth Musau. Ugependa kuongea? Mwaisha Munyooki.

**Mwaisha Munyooki:** Thank you Madam commissioner. Mimi nigepele kuongea juu ya haki za wanawake, haki za wanawake.

Jambo la kwanza lile ningependa kuongea juu ya haki za wanawake, kwanza ni security and peace. Unaona hii ikokatika kipengele cha A.23, cha African Charter. Kila mwanainchi ama awe na haki za peace and security.

Ile ingine ningependa nini, kueleza juu ya nini, yaani kutoa maoni juu ya wanawake, ni juu ya wanawake vile wanatumiwa katika familia. Unaona, mwanamke hawezi kuruhusiwa kutumia, ama kuchukuwa vyombo vya nyumbani. Vitu kama ni shamba, kama ni ng'ombe iko kwa hiyo nyumba, ama nini, mwanamke aweze kuruhusiwa kutumia hiyo kitu, pasipo ruhusa ya mwanamme. Kwa hivyo, katiba hapo, yaani iangalie sana juu ya wanawake.

Ile ingine, yaani wanawake katika familia wanatumiwa kama chombo tu, kama kupitia tu kwa wazee wetu, mabwana na wazazi. Wazazi wa kiume I mean. Yaani, fathers and husbands, wanawake tunatumiwa tu kama chombo katika hiyo nyumba. Kwa hivyo katiba, yaani izingatie sana juu ya wanawake.

Ile ingine ningetaka, ni wanawake wawe na rights za kutumia hizo vitu tuseme. Wachukuwe hivyo vitu wavitumie, wawe na haki ya kutumia hivyo vitu pasipo kuchukua mawaidha kutoka kwa wanaume, kwa maana hao wanajitoleshea pia kwa nini. Yaani kwa mmmmmhu.

Haya, ile ingine ni to work in a safe environment. Wapatiwe kufanya kazi katika mazingira yalio safi. Wawe hawaingiliwi yaani I mean. Hawaingiliwi, na kimaumbile, yaani I mean sexual function zao ziwe considered sna, unaona, wasitumiwe vibaya na wanaume, hiyo pia katiba ihusishe wanaume.

Ile ingine ni equality in education na nini, na kama ni colleges ama nini, wawe wako na equality.

Ile ingine ni upande wa politics. Wanawake wausishwe sana katika nini, yaani wahusike sana katika siasa, politics I mean, siasa. Wanawake wapatiwe nafasi sana katika siasa, wawe na percentage iko juu, kwa maana naona ile percentage wamepatiwa katika siasa ni kama one third. Sasa waongezewe iwe ni kama 50%, katika siasa. Wanawake.

Ile ingine ningetaka kuongea juu ya wanawake, ni rights ya kupatiwa heshima na kulindwa, ulinzi, yaani wawe na ulinzi wanawake, waheshimiwe tena walindwe. Hata kufikia katika nini, kiwango cha kule nyumbani, wanawake wale wa chini kabisa wawe na ulinzi, kwa maana tunaona wanawake, saa hizi, mwanamke akipigwa hapa inje, aende polisi, utasikia akiambiwa hizi kesi ni za nyumbani rudi nyumbani. Hapana, wanawake wawe considered.

Ile ingine ningetaka ni right ya enjoyment; unaona, wapatiwe haki katika kufurahia kila kitu chochote hapa inchini. Wawe na haki ya kufurahia kila jambo, wasizuiwe, waambiwe ati kiwango cha wanawake ni fulani, wawe uhuru.

Ile ingine wapatiwe freedom of movement. Wapatiwe uhuru wakutembea na residence, na wakuishi mahali popote.

Ile ingine ningependa katiba itilie manani, ni katiba iwe translated kwa lugha zote za Kenya, kila mkenya yaani awe ameelewa

katiba ni nini. Kwa maana kama ingekuwa ivyo atungekuwa na civic education na nini. Kila mtu angekuwa anajua katiba ni nini.

Ile ingine ni katiba iwe kama subject katika skuli zetu. Ni hiyo tu asante.

**Speaker:** Subiri tafadhali, tafadhali subiri.

**Com. Abida Ali:** Ningependa utufafanulie, unasema kwamba wanawake wanatumiwa kama chombo, na wazazi na waume, na ungetaka katibe iangalie. Sasa ukiongea namna hivyo atuelewi, tunataka utufafanulie. Unataka katiba ifanye nini, kwa sababu ukisema wanatumiwa kama chombo na katiba iangalie, pengine wengine atuelewi

**Mwaisha Munyooki:** Unaona kutumiwa kama chombo ni hivi; unaona wewe ni mwanamke na for example umeolewa na mwanamume, si ndiyo. Sasa ndio umesikia niki sema wanatumiwa kama chombo, to be passed between husbands and fathers, unaona? Sasa unachukuliwa wewe ni kama mbunzi ya nyumba hiyo tu, uchukuliwi kama wewe ni mtoto katika nyumba hiyo

**Com. Abida Ali:** Unataka katiba ifanye nini?

**Mwaisha Munyooki:** Sasa tunataka katiba ipatie wanawake uhuru, katika uwana. Tuseme kama affirmative action.

**Com. Abida Ali:** Zura Hassan? Zura Hassan ni nani? Hauna maoni, okay. Na Asha Zubira una maoni? Okay. Joseph Nzioka?

**Joseph Nzioka:** Asante sana

**Translator:** Ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniongoza kufika hapa. Kuona waheshimiwa ma commissioners. Mimi nashukuru sana kwa sababu sijawahi kusimama mbele ya watu kama leo, na ninashukuru kwa sababu leo nimeruhusiwa kusimama. Mimi nataka kusema neno juu ya Kenya.

Mimi ni mmoja wao wale walikula kiapo cha maumau. Nilikula kiapo nikitafuta mchanga wa Kenya, na sijauwona. Nina sikitika sana kwa sababu, nikiangalia wale tulitaabika na wao, tutafute uhuru na mchanga wa Kenya pamoja, na hatujaona huo mchanga. Nikikumbuka marehemu mwanzilishi wa taifa ile la Kenya, pamoja na watu wetu wengine walio kufa mbeleni, tulikuwa tunapigania juu ya mchanga, na hatujauona. Nauliza serikali yetu ambaye imetuita leo ili tuje kuandika katiba ya kesho, itutafutie kile tulikuwa tunachotafuta sisi wakenya. Je mtu anaweza kuchokeshwa na kitu na akatae kukila?

Mtu akichinja mbuzi, anatakiwa kula kichwa, mara, kila kitu mpaka hata na mguu, na kila sehemu ya hiyo nyama, kwa sababu amechoka kuchinja. Swali ambalo naweza kuuliza ni hili; Tulipokula kiapo tukitafuta mchanga huu wa Kenya, tulikuwa tunataka

kuutafuta tuupate, na hatujaupata mpaka wa leo. Naomba serikali ambayo tunaanza kuunda sasa, itutafutie sisi, ma ex-freedom fighters, acre hamsini kila mmoja. Nauliza serikali yetu kwa wale waliopigania uhuru wetu, wengine walikufa wakawacha watoto wao na watu wao, na hawajapatiwa chochote, tunaomba watafutiwe kitu, katika kule kupigania uhuru wetu. Naomba katika wale freedom fighters, wengine walikufa, wengine tuko na tuko na shida, na tungeomba hiyo serikali ambayo inakuja, baada ya kuunda hii katiba, kwa sababu ninashukuru, ma commissioners wetu, viongozi wamekuja, ili kila mmoja wao, hao watu waliopigania uhuru wetu, watafutiwe na serikali milioni moja.

Ya tatu, naomba serikali inayokuja itambue ex-freedom fighters katika pre-amble yetu, kwa sababu kama hatungepigania uhuru wetu, uhuru ungepatikana Kenya. Asante. Tunaomba tutafutiwe katika district level au divisional level, tutafutiwe pahali ya kuwa tukikutana wakati ule tunajadiliana mashida yetu sisi watu wa Mau mau, kwa sababu sisi ni masikini hatuna kitu. Asante.

Iko kitu ingine nitasema ya Kikamba; kuna mila ya Kikamba ilikuwa inatumika amani, na ilikuwa inaitwa, 'kithito' kama mtu amechukuwa mali yako au amekataa na mali yako, kuna kitu ilikuwa inaitwa 'kithito' ambayo ilikuwa inakuliwa. Ikiwa mtu amechukuwa mali yako, alikuwa napigiwa hii 'kithito', anakufa yeye na watu wa ukoo wake, kwa sababu amekataa kulipa mali yako. Mtu akikataa na mali ya mwingine, alipopigiwa 'kithito' alikuwa anakufa.

Nimesahau kusema mambo ingine ya wasichana wetu ambao wanacheza na vijana. Msichana alipowekwa mimba na kijana, na huyo msichana akufu na hiyo mimba, zamani, wenye huyu kijana ambaye aliweka mimba msichana, walikuwa wanamlipa, zamani. Alikuwa kabla hajalipwa, hiyo mimba ilikuwa inapasuliwa, ijulikane mtoto ambaye amekufa ndani ya huyu msichana ni msichana au ni kijana. Kama ni msichana alikuwa analipwa ng'ombe sita, kama ni kijana, analipwa ng'ombe saba. Mwanaume alikuwa analipwa ng'ombe kumi na nne, na mwanamke ng'ombe kumi na mbili. Sasa, sisi tunakaa mbali sana na serikali, tunakaa ni kama tumesahauliwa, na tunaomba mfalme ambaye atakalia kiti, akumbuke sisi, na akalie kiti na atawale inchi hii, kama vile Moses alisimamia wana wa Israeli. Tulipo kula Mau mau, tulimwaga damu, ili usalama uonekane, na hatutaki tena kuona damu ikimwagika, na tunaomba atakayetawala atawale vizuri, ili tusione damau ingine ikimwagika. Asante sana.

**Com. Abida Ali:** Kuna swali mzee, subiri tafadhali.

**Speaker:** Unajua hukutuambia tutafanya nini na kithito.

**Joseph Nzioka:** Kithito, mtu kama anakula mali ya watu, kama mimi nakula mali ya mtu na nikatae nayo, nitakwenda kupikiwa kiapo.

**Speaker:** Okay asante. Na ingine. Hii ya mvulana akiweka mimba na ameruka msichana, unataka tuanze ku, tufanye nini

**Joseph Nzioka:** Tufuate mila zetu

**Speaker:** Ooh Wakamba wafanye mila zao

**Joseph Nzioka:** Ndio.

**Speaker:** Na wengine

**Joseph Nzioka:** Wafanye mila zao

**Com. Abida Ali:** Asante's mzee. Mustafa Haji?

**Mustafa Haji:** Okay asante sana. I would like to speak about one issue, and that is about the Chief Kadhi. The Chief Kadhi should be elected by the muslims but not appointed. And it should be seen that all matters that pertain to Islam, should role according to the Islamic Law, and should be well versed with the Islamic sheria.

On qualifications; he should have all the qualifications of other Chief Justice.

Again I will speak about the youth, especially the H.I.V Aids orphans. They have actually been isolated in the society. So we would like to, since we have a ministry that looks into all this issues, like to appeal to them that in the new constitution they should be recognized and given the assistance required. Na youth ambao hawana kazi, we have so many youth who are running up and down. Wengine wamesoma mpaka university. So, katika new governance that we want, kama tuko na chief, for example I will start with the councilors; councilor, I will recommend councilor awe ana degree, because we have so many young people moving up and down with degrees na hawapatiwi hizo chance. M.Ps at least wawe na masters, because hatutaki kuwa na dormant government, itatuingisha kwenye mashimo. So we would like to appeal, all M.Ps should have Masters' degrees.

And the president; the president also should have higher qualifications than the M.P, and there should be separation of powers. The president should have his powers, not the president and again the M.P, and if it is possible, let him hold a PHD, because we are moving with time and people are now educated. Hauwezi ongoza watu na una elimu, that is one.

Again, I don't see the work of the local administration. For example, when you are taking an I.D card, you are going through a very long process. The Sub-chief has to sign, the Chief, the D.O, the D.C, all that procedure. So, we should have one person to sign for all this documents. If it is the D.C, the D.C only. Again, I don't see the work of the Chief and the Sub-chief, afadhali tuwe na mzee wa kijiji ambaye analipwa, and again elected not appointed.

Na la mwisho; the issue of I.D cards. There is a lot of discrimination, especially, I would say, if your name sounds Islamic, it becomes a problem again for you to get an I.D card, or even birth certificates. So, the procedures should be looked into, na mambo yawe rahisi. Thank you very much.

**Com. Abida Ali:** Jackson Wambua? Jackson Wambua? Rhoda Ndungu? Jackson Wambua ungetaka kuongea? Okay.

**Jackson Wambua:**

**Translator:** Mimi nashukuru sana kwa hii tume ya katiba, kupewa hii nafasi ya kusema.

Point yangu ya kuanza kupeana; ni haki yetu kwa kuwa kutoka kwa akina babu zetu, tulikuwa na haki yetu ya mchanga, hata kitambo, kabla mzungu kuja. Na tuna stahili kurudishiwa hiyo haki yetu ya mchanga. Kila mtu awe na pahali pa kuishi, kwa sababu shida mingi katikati yetu sisi hapa ukambani ni mashamba.

Point ya pili ni mambo ya utawala. Maoni yangu ni, kutokea D.O kuteremka mpaka mzee wa kijiji tunastahili kuwachagua na kura. Kwa upande wa utawala, kila mwanainchi anatakiwa kupewa haki yake na hawa watu wa utawala ambaye amewachagua.

Point ya tatu, ni upande wa elimu. Tunastahili kupewa elimu ya bure kutoka kilasi cha kwanza mpaka cha nane. Na serikali isimamie kama vile ilikuwa inafanya mbeleni, ipeane vitu, vyombo vile vinatumika shuleni, na pia mijengo ya shule, yenyewe ijenge. Na Headmaster awe hana uwezo mwingi katika shule, uwezo ubaki na wazazi.

Upande ule mwingine wa nne, ni upande wa kusaidiwa na serikali. Katiba ambayo tunatengeneza ya serikali mpya iangalie, tupewe maji bure na hospitali iwe bure, na iletwe dawa ya kutosha. Kwa sababu mwanainchi wa chini wa kawaida, awezi kujimudu, kuweza kununua dawa ambazo ziko bei kali sasa, wengi wanaumia wakiwa nyumbani kwa sababu hawawezi kununua dawa, ambazo ziko na bei kali.

Upande wa hospitali pia. Inatakiwa kila sub-location iwe na health centre au dispensary. Kwa sababu wakati huu kuna diseases nyingi ambayo ni communicable kwa local people.

Upande ule mwingine ni upande wa councilors, wabunge na president. Councilor awe mtu wa elimu ya chini kiwango cha O' level, asiwe akawa mtu wa degree. Na huyo councilor ambaye anachaguliwa awe mtu wa kuaminika kutoka area yake, na akimaliza miaka mitano, ikiwa ajafanya makosa anaweza kurudishwa tena, au akifanya makosa, wanainchi watafute mwingene.

Upande wa mbunge; awe ni mtu wa kutoka elimu ya kiwango cha kutoka katikati ya form four na degree, na awe mtu

anajulikana katika division yake, pahali anatoka. Na akifanya makosa, wakati yeye yuko, anaendelea na hiyo kazi kipindi chake, mwanainchi anafaa kuruhusiwa atafute mjumbe mwingine. (Interruption)

**Com. Abida Ali:** Tafadhali jaribu kufupisha.

**Jackson Wambua:**

**Translator:** President anafaa kuwa na degree. He should declare his wealth first, na election for the president should be alone, separate from that one of the parliamentarians. Maoni yangu inafika hapo asante.

**Com. Abida Ali:** Asante sana, na nilisahau kuwajulisha kwa commissioner mwingine ambaye ameungana na sisi, ama mnaona ni kijana, pengine hamkujua ni commissioner. Anaitwa Isac Hassan, na kwa wale ambao hawakuwa wakati tulifanya introduction, tulikuwa watu wachache sana. Karibu na Hassan tuko na Prof. Wanjiku Kabira, alafu mimi naitwa Abida Ali-Aroni. Na masharti ni kwamba tukikupatia nafasi, tafadhali ikiwa hauna memorandum, jaribu kuongea chini ya dakika kumi, kwa sababu saa ingine tunaona aibu kuwakataza, kumaliza maoni yenu. Ikiwa una memorandum, tafadhali, dakika tano, ili, tunaona mmezidi, na tungetaka kila mtu aweze kuzungumza. Tumeelewana. Asante. Paul Muthama, Village Elder, watu wametuongua sana habari ya Village Elder, tunakuaribisha uongee. Dakika tano, tafadhali.

**Paul Muthama:** Commissioners na tulio hapa, ni asante kwa hii nafasi ambayo nimepatiwa, nizungumze ijapokuwa nimeambiwa kama habari ya village elder imezungumzwa.

**Com. Abida Ali:** Ongea kabisa vile unataka.

Paul Muthama: Nitaweka point mbili, tatu hivi, zingine zemewekwa, zimezungumzwa. Vile ambavyo nilikaa na wazee wengine, tukaonelea ikiwezekana katika pre-amble hii, vitu viendeleo na kuwekwa, hili village elders wawe wanaonekana ni kama watu viongozi wa msingi. Ni, kwanza wachaguliwe na kura, lakini si kuchaguliwa na Assistant Chief, ama mtu mwingine kwa mapendeleo. Awe akilipwa, wajua yeye ni mfanyi kazi wa serikali kama wale wengine. Awe anajua kusoma, sababu ya kusema awe amesoma, ni kwa vile anatakikana kuenda katika kamati ya shule ya primary, lakini hawaitwi, kwa sababu mtu ambaye ajasoma, atakuja kusema nini katika education. Awapatiwi nafasi ya kuzungumza habari ya wanainchi ama wazazi. Na wapatiwe kitu fulani ambacho kitakuwa kikionyesha akiwako katika wale wengine, kama Assistant Chief ama Chiefs wamepeva uniform, budges, unajua huyu ni Chief, unajua huyu ni nani. Lakini wazee wa vijiji wamewekwa hivi tu, lakini ndio waanzilishi wa utawala katika national. Wapewe heshima ya kutosha, kama vile tunavyo wapatia Provincial Administration wengine, na wakikosa kuheshimiwa kama hivyo nimesema, utaona maendeleo yanadidimia. Tangu utawala, utaona watu waliozaliwa tangu wakati wa utawala, wamesoma na wako karibu ku-retire, sasa kukiwa kama vile zamani, ya mcolony, mzee anachukuliwa ambaye ni mzee wa tobacco kama kikamba, ananyuza. Utaona hata waliosoma, hawampatii nafasi, apewe heshima, lakini kama akiwa amesoma, hata atapewa heshima na wale ambao wamesoma, ambao wanasema wako kazini,

wengine watastaafu. Asante.

**Com. Abida Ali:** Asante. Elizabeth Musau. Angetaka kuongea, Elizabeth Musau, okay. Elijah Kimanthy?

**Elijah Kimanthy:** Asante sana. Kwanza nawashukuru kwa nafasi hii nimepata, ili nitoe maoni kidogo.

Kwanza ningezungumzia juu ya pre-amble. Katiba yetu mpaka iwe na utangulizi. Ionyeshe wapigania vita wetu, tuseme freedom fighters, kama vile Mau Mau, kwa nini iliundwa, na iliundwa na nani, na iliundiwa wapi?

Alafu nitazungumzia juu ya uraia. Raia wa Kenya, awe ni ule amezaliwa Kenya, wazazi wake wamezaliwa Kenya, na wengine kama wametoka inje wanaweza wakajiandikisha kupitia taratibu zinazoitajika, ili wawe raia wa Kenya.

Nitazungumzia juu ya haki za raia. Kila mwanakenya, sababu tulipigania uhuru ile tupate haki hizo, kwanza mchanga. Kila raia wa Kenya awe na mahali pa kuishi, kulingana na sheria, labda apewe hekari ishirini, kila mmoja, mwanamke kwa mwanaume. Tuseme government land, zipunguzwe ziwe zinatimiza wajibu tu, kwa tuseme research, kama National Park, zisipunguzwe ile zitosheleze wanyama wale ambao watatumika tu kwa tourist, peke yake. Sehemu zingine zigawanywe kwa masquatters. Hatutaki pia kusikia jina masquatters inchini Kenya sababu tulipigania uhuru, na tulipigania mashamba, hasa sana, maana tulinyang'anywa mashamba na sheria za ukoloni.

Nitazungumzia juu ya utawala. Sioni kama pana haja ya kukuwa na Provincial Administration, maana tulichagua watu kutoka councilors, M.Ps, na tuseme president. Hatuoni haja ya hawa wengine, maana wamechaguliwa na mtu tu, hatujui wameandikwa kupitia njia gani? Labda waliletwa na mzungu akiwa anataka kutumia ile amri yake ya divide attitude.

Ningependa kuzungumzia zaidi, juu ya elimu. Elimu ipewe free kwa wote. Kama ni maji, maji ipatikane kwa wote, saa hii nimezungumzia haki. Haya, kama ni mambo ya madawa, hospitali ziwe kila mahali kwa location levels, tuseme. Dawa zakutosha, madaktari wa kutosha wapatikane, maana tumechanga, yaani tumetowa kodi.

Kile kingine ningetaka kuzungumzia ni succession of powers. Wakati wa uchaguzi, president, kama president ame retire, hana haja ya kupewe chochote. Enyewe apewe security na awe anaweza kupata, tuseme pension kidogo tu. Security kama bodyguard wawili, gari na pension. Lakini wakati wa uchaguzi, Attorney General ashikilie kiti. Si ati awe amekaa kando na huku wanataka kuchaguliwa. Ni hayo tu, sina zaidi.

**Com. Abida Ali:** Asante. Gichuri Karanja Kabono.

**Gichuri Karanja Kabono:** Thank you. Thank you commissioners and other distinguished guests and ladies and gentlemen. I



have about three things to talk about to the commission.

One; it is about the commission of lands; the other is about the president. The third one is the government make-up, and the fourth one is education.

Commission of lands should be scrapped off. They created no lands, but inherited from the colonial rules, and because of that they have been able to dish lands anyhowly regardless of the poverty within the local people. How the commission of lands in Nairobi understands the problem at Mtito wa Ndei, Wangaitethia, he does not understand anything, and as a result this question of land, should be brought down to the owners. Commission of land is the creator, is the father and the mother of squatters, and it should be replaced with elected officials within the divisions and any land dispute should not go beyond the district level. On the mean time in order to cut the land grabbing, excess land, depending on the area, should be taxed, and the revenue be returned and counted for by the local authority.

Having cleared with the commission of lands, I will talk about the office of the president. For the 37 years, we have been independent; all this periods have been utilized by the commissions, and should have been not utilized if we never had excess of power by our past two presidents. Our first two presidents are only answerable or have been answerable to only two powers. One, God. The second power is another president of another nation in case of war. Other words, they have never been answerable to either the parliament or to the wanainchi, and the constitution we are talking about, it should be set in such a way that the president will be countable, will be answerable and would be punishable by the law. There is another view that the president should run for only one term. That is, if we have the right parliament, then we do not need the president to run for various terms, simply because for the first term, he runs how to handle the office, and when he comes to the second term, he prepares himself for life presidency, and the future generation will be happy to see five to ten retired presidents. Mmoja ameenda, amerudi kwa chang'aa, anakunywa huko, mwingine amekuwa sales man, mwingine amefilisika ni mlevi na wengine ni watu wa maana. Utamu wa hii kitu ndio imefanya inchi yetu iharibike, na president akijua ya kwamba akimaliza miaka mitano ni out, taabu yetu inapunguka. Papo hapo ndipo nitaongeza, one man one job. Tukichukuwa kama president wetu, yeye ni mbunge, ni President, Prime Minister, Commander in chief, Chancellor of all universities, this is too much.

In civil service, that is local na ingine ya juu, one man one job. Pamoja na hayo ni, kama president anawacha kiti kwa kuwa disabled au kwa kitu fulani, yule ambaye atafikiria ili kipate mwenyewe asiwe candidate ya hiyo kiti kinakuja. Otherwise, ata wewe ukiwa unakwenda kushikilia ni kwa nini ukubali mwingine akalie na umesikia utamu?

Ya tatu. Ni mhubiri wa serikali. Kwa mfano ikiwa tunachaguliwa na watu kumi na sisi ni wawili, tano kwa tano tuko sawa, mmoja apunguke upande wa kwangu, upate sita na mwingine apate nne. Umemshinda na mtu mmoja tu, ni kwa nini hawa wa nne wasifikiriwe. In other words, wewe unapata watu sita uwe president, na wewe ambaye umeshika watu wanne uwe ni vice president, na vile vile watu wako wapatiwe viti kulingana na proportion za kura, simply because, we should start thinking in

terms of doing this for the better of Kenya, not for certain regions or certain people, good for the Kenyans.

Ya nne na ndio ya mwisho, ni elimu. There should be only two categories of school; government and private. Kama mahali tuko, P.C wameanza shule yao, kutoka nursery mpaka university, ni yao na ni private. Mugoya vile vile, hata mimi individual nikitaka yangu private, niaanze kutoka mwanzo mpaka mwisho, lakini si nikifika katikati, serikali ingaingia ati inaleta walimu na kadhalika. Nayo serikali iwe na shule zao. Hapa mimi ninalinga hii kitu ambaye kilirudi juzijuzi inaitwa sponsorship. Ikiwa shule ni ya P.C.E.A, they are the sponsors, it is their property. Serikali ijenge yake ingine kando mahali pengine, ili iwe inashindana na hii. Na pamoja na hiyo, pawe shule za kuhudumia walemavu. Ziwe za serikali na vile vile, hata private, sababu hata wao wako na walemavu. In other words, shule iwe ya serikali ni private. Ma commissioners, nimemaliza hapo, asanteni sana.

**Com. Abida Ali:** John Kilonzo?

**John Kilonzo:**

**Translator:** Nami nawashukuru nyinyi ma commissioners ambao mnashikilia huu mpango wa katiba. Nitasema maoni ambayo niko nayo kuhusu mashamba.

Tangu tujitawale, vile serikali ilikuwa inashikilia mambo ya mashamba, hata sasa baada ya kujitawala ni hivyo vivyo. Sisi wanainchi wa kawaida, hatuna uwezo wa kuingia kwa hiyo mashamba, lakini serikali inachukuwa hao watu wakubwa, wanaingizwa kwa hizi mashamba. Na mwenye inchi ambaye ni squatter, anakosa pahali pa kuishi. Naona inafaa kila mwanainchi ambaye alipigania, ambaye yuko Kenya, pahali tulipigania uhuru, apewe sehemu ya inchi, ambaye inafanana na yule mwingine. Hata Mungu aliweka mpaka ya kikabila vile kila kabila inaishi. Kuna mpaka hapa ukambani, inasumbua sisi katikati ya kabila ya wakamba na wamasai. Kwa sababu Maasai wanasema mpaka wetu na wao ni railway line, na sisi wakamba tunasema na tunaamini kwamba mpaka ni mto inaitwa 'Kwa Katue'. Katue alikuwa mkamba, huyo mto sehemu hiyo ilitwa, mto uliutwa Kwa Katue, kwa sababu aliyekuwa anaishi uko, alikuwa mkamba alikuwa anaitwa Katue.

Nitasema kidogo juu ya elimu. Tunatakiwa kutengeneza mpango wa elimu vizuri, watoto wa kike na wa kiume, wote wasome bila kubaguliwa. Kisomo kinaleta shida kwa sababu ya umasikini ulioko. Kuna watoto wengi ambao hawako masomoni sasa kwa sababu ya kukosa fees. Ningetaka hii katiba iangalie hao watoto wanaweza soma namna gani kwa sababu wazazi hawana nguvu.

Huku Kibwezi, hatuna Title Deed, lakini tuna makaratasi yanaandikwa number ya hiyo mashamba, na tungeomba tupatiwe Title Deeds, ili tuwe na uwezo wa kuenda kukopa pesa kwa serikali.

Ile nitasema ni kuhusu administration, kutoka juu mpaka chini. Kufikia wazee wa vijiji. Village elders ndio wanafanya kazi

nyingi, na ni wa kiwango cha chini, na ndio wako na

raia na hawalipwi. Naomba village elders waangaliwe, Kenya mzima, si hapa Kibwezi peke yake. Mimi nashangaa sana, wajumbe wanazungumza kwenye parliament na wanaonekana hawafikii vizuri juu ya mshahara wa village elders. Nao village elders ndio wana mambolise raia ili wajumbe waweze kuchaguliwa na waweze kufikia hiyo raia. Na wajumbe sasa wanaanza kupigania mshahara kubwa, yao wenyewe, wakisahau village elders. Nashukuru asanteni sana.

**Com. Abida Ali:** Asante. Mbindyo Mutu? Mbindyo?

**Mbindyo Mutu:**

**Translator:** Mimi nashukuru sana kwa sababu, sijasimama mbele ya watu kama vile tulivyo leo, tangu tujitawale, kwa hivyo nashukuru sana.

Mimi nitasema juu ya Maumau kwa sababu mimi ni mtu wa Maumau. Tulipo kula kiapo ya Maumau tulikuwa tukitafuta mchanga, na mchanga ndio huu nashika. Na, tulipokuwa tukikula kiapo, tulikuwa tunashika mchanga hivi tunavyo shika sana. Tangu tufukuze Mwingereza Kenya, tangu tutawale, hakuna mtu amewai kujali masilahi yetu sisi watu wa Maumau, na sisi ndio tulipigania hii uhuru. Na matunda yanayo kuliwa Kenya, ni sisi tulitafuta. Kwa hivyo serikali ilioko sasa imesahau habari yetu kabisa, na tukabaki huku kwa milima. Na tulipo pigania uhuru tufukuze mbeberu, sasa tena Kenya kumerudia mbeberu mwingine amekalia viti. Sasa, tunaomba sisi watu wa Maumau, tutafutiwe our reward, ambaye itatutosha kwa ile kazi tulifanya, kutetea uhuru. Mimi sitasema sana, kwa sababu wakati ninaposema, kichwa yangu inawaka moto na ninaweza sema maneno mabaya. Lakini nasema tukumbukwe pale bungeni. Asante, mimi nafika hapo.

**Com. Abida Ali:** Asante sana mzee. Joshua Kavivya?

**Joshua Kavivya:**

**Translator:** Leo nina furaha kubwa sana siku ya leo. Kwa sababu katiba inayotutawa ilitengenezwa kule Lancaster House, na leo serikali yetu imekubali katiba tuje kuunda hapa hapa kwetu, na ikatengeneza tume. Commissioners ambaye wako hapa, nafurahi sana kwa sababu yenu nyinyi. Kitu ya kwanza tulichokuwa tunataka, ni serikali. Kile kingine tulikuwa tunataka, ni mchanga. Kile tulicho nacho ni what we call in English gardens not the pieces of land. Kwa hivyo mchanga wetu uliochukuliwa na mzungu, ndio tunataka, kwa serikali inayo kuja. Vile tulikuwa tunapakana, mipaka ilikuwa inakaa, kutoka mlima wa Chulu hills mpaka Tsavo, hiyo ni inchi ya mkamba. Na ilie umasikini tuko nayo ya mkamba, kwa sababu mkamba hana pahali ya kufanyia kazi. Watu wako hapa, walinyang'anywa inchi kabisa, inchi ikawa ya watu fulani. Watu wengine wa acre kumi, na wengine wa acre mia mbili, na tunataka tuwe equal. Tunataka kuwa equal. Kwa sababu hii inchi yetu ni ya jua, na kunanyesha one season, na inchi ni mbaya. Tunataka kila mtu apewe kama acre hamsini, ili ukilima mvua ikosekane, uchungu mbuzi, upate mali. Na hatutaki hii acre hamsini tuwe masquatter, tunataka hii katiba tunayounda kwa serikali itakayo kuja, mambo ya masquatter ikwishe kabisa, ikwishe kabisa.

Nakujia sasa kitu ingine kinaitwa kisomo. In Eastern Province, we have no university. Na watu leo wanashibishwa na university. Watu hawana university hawana elimu, na tuko na shamba hapa, ilichukuliwa watu wakanyang'anywa, wakaambiwa ni university, lakini ni ya uwongo. Ikiwa ni ya kweli, we want a full university here, tunataka university hapa.

Kingine mimi ninataka kuongeza ni; na mnivumilie sijui nitaona nyinyi tena wapi. Kitu nataka kusema ni hii, hapa hakuna hosipitali. Hosipitali iliyoko hapa iko Makindu, na kilichoko hapa ni Dispensary. Na hapa tunataka hosipitali iliyo na kitanda mia mbili, ward ambayo iko na kitanda ya kulala wagonjwa mia mbili na arubaini. Na ile shambe iko hapa ni acre mbili, kwa nini na inchi ni yetu? Kwa nini hapana jenga hosipitali mbili na inchi ni yetu? Tunataka tupewe shamba ya kutosha, tujenge hosipitali. Hapa hakuna kaburi ya kuzika watu wakikufa, na kama nadanganya watu wa Kibwezi wako hapa. Ni kweli ama si kweli?

**Crowd:** Ni kweli.

**Joshua Kavivya:**

**Translator:** Hakuna pahali pa kuzika, hakuna kaburi ya kuzika watu wamekufa. Tunataka tukimaliza kutengeneza hii katiba mpya, serikali itakayo kuja, county council yetu, ikate kiwanja kinatosha kujenga hosipitali na ingine ya kuweka kaburi.

Mjumbe wa parliament; mtu wa parliament anatakiwa kuwa mtu ako na degree, hapana form four. Wengine ata ni form four failures. Tunataka mjumbe university mtu yuko na degree. Atatengeneza katiba na sheria zitengenezwe na mtu anajua sheria. Haiwezi kutengenezwa na mtu wa form four, hivyo ndivyo naona.

County Council, Councilors, tunataka mtu anaweza kuchaguliwa kuwa mayor, atachaguliwa na watu, uchaguzi wake uwe wa kila mtu. Mtu yuko na knowledge. Hiyo ni maoni yangu. Wacha ni geuke pali pengine.

Mambo ya kutawalwa; kutoka kwa president, kwa sababu president ni mtu wa high level, akae hapo peke yake, na achaguliwe na watu wote. Na, si yeye atakayechagua his Vice. Vice president achaguliwe na watu wote, kwa sababu akiwa ni mtu wake, atakuwa akumfanyia yeye kazi. Tunataka Vice president awe anatumikia watu na achaguliwe na watu. Hapo nitafika hapo.

Ngoja nigeuke kwa disabled, kwa sababu mimi ni mlemavu. Mimi ni mwenyekiti wa Kibwezi ya walemavu. Tunataka kitu ya kwanza, serikali ijenge shule ya visiwi, wale watu ambao hawakisii, deaf. Kwa sababu watoto ambao ni deaf, hawafunzwi vizuri. Na waletwe walimu ambao wanaelewa hii lugha ya deaf. Nilikuwa Mombasa, na kule Mombasa niliona shule ya blind, watu ambao hawaoni. Na niliona mwalimu anajua kufunza hao watu hawaoni. Huyu mwalimu ni shwari kabisa. Na kwa sababu kutoka hapa mpaka Mombasa ni mbali, tunataka pia ya vipofu ijengwe hapa karibu, ili watoto wetu vipofu wasomee karibu. Na hao watoto ambao hawasemi, shule ya dumb iko Mwingi, tunataka moja iwe hapa Makueni district. Ili watoto

wetu wafunzwe na hao watu waliosoma hicho kisomo cha dumb.

Kingine naona kiko na shida hapo, ni habari ya bursary fund. Tunataka serikali itakayokuja baada ya kuunda hii katiba, iwe ikipeana bursary fund vizuri. Kwa sababu watoto wako Mtito Division, Kibwezi Division na Makindu Division, hawapewi bursary fund vizuri. Na bursary fund inagawa na ma councilors, na hakuna councilor anafikiria hao watoto. Na tunataka wale ma councilor wataenda kwa councils, kwa council zetu, wajue kwamba hawa walemavu wote, wawe viziwi, wawe vipofu, wawe dumb, ni watu kama wale wengine.

Ya nne katika walemavu, nataka ichukuliwe censors ionekane ni wangapi. Kwa sababu hata wanyama wa mzituni, hawa wa K.W.S wanajulikana ni wangapi, lakini viwete hawajulikani. Hata nyani wanajulikana ni wangapi, hata katumbili wanajulikana ni wangapi, lakini walemavu hawajulikani ni wangapi. Tunataka tuwe classified, tuwe pahali pamoja na tujulikane. Wakati wa councilors wanao chaguliwa sasa, na ma Members of Parliament. Tuna 210 Members of Parliament in Kenya, na tuna Province nane. Tunataka watu wanane, Members of Parliament, hiyo viti iwe wazi, iwe ya walemavu, iwe anaingia unopposed. Iwe hakuna shida. Hiyo ndio maoni yangu mimi.

Na katika council, nyinyi wanaume ambao mnaishi huko councils, Kavivya awe akipambana na wao, akichaguliwa councilors. Na tunataka tuchaguliwe councilor mmoja kama mimi katika council so that wakati tunagawa vitu vya council, igawe, walemavu wapate haki yao na hao watu wengine wapate haki yao.

Iko shida ingine ya disabled; iko watu wakubwa walemavu, na hawana njia mzuri ya kufanyia haja zao hiyo ya kitandani, tunataka serikali itenge pesa ya vitu vya kusukuma hao watu, wakati wana haja waende haja vizuri. Kwa sababu sio mapenzi yao walizaliwa hivyo, hawakutuma application kwa Mungu wazaliwe walemavu. Hiyo ni maumbile. Tunataka hii kitu iwe sawa.

Iko kitu ingine nataka kusema. Mambo ya akina mama.

Unajua sasa kuko na ukimwi, hao watu ambao ni wazima wanakimbia kwa viwete, watimilize haja zao za sex, na unajua mlemavu asema sana, tunataka ulinzi wa walemavu uwe mzuri. Mtu mlemavu akishikwa na mtu ambaye ni mzima, akiletwe polisi, iwe hakuna corner. Na mimi nikifika hapo naona kama ni vizuri, kwa sababu naona mambo hayawezi kuisha hapa. Unisamehe commissioner, unipe dakika moja tu niseme moja ya kisomo.

Ile primary schools ambazo tuko nazo hapa, uwanja ni wa serikali na kama ni shule ilijengwa pahali, hatutaki iwe ni kama bahati mbaya ilijenga hapa. Ilijengwa na shule ni ya serikali. Na ikiwa ni shamba ya mtu ambaye shule imejengwa aende akatafutiwe pahali pengine. Shule aiamehwi, na wazazi hawana pesa ya kulipa pesa. Nikifika hapo ni sawa kabisa nasikia raha. Asante.

**Com. Abida Ali:** Asante sana. Jonathan Munuve? Yuko? Usipitishie dakika kumi tafadhali. Kama ukifanya saba itakuwa afadhali.

Jonathan Munuve:

Intepretor: Mimi naitwa Mbalu Munuve. Mimi nina miaka sitini na nne, 64 years. Mimi nashukuru kwa Mungu na serikali ya Kenya. Kutoka tulipojitawala wakati wa mzee Kenyatta na Paul Ngei, hawa ndio waliwafukuza mbeberu hapa, na wakachukua kifagio wakafagia hii, na wazungu wakaenda. Na wakati huo tulikuwa bado tuko squatter, na sasa tuko squatter. Hii ikiwa ni katiba ya kweli, naomba mambo ya squatter ikwishe kabisa. Sasa nikiambiwa mzee kama mimi ni squatter, hii ni kama kuni decolonise.

Ingingine sasa hiyo imekwisha, sisi tunataka mashamba, shamba tu tunalia shamba. Wengine wana acre tatu na una watoto sita ama kumi, tupewe mashamba ya kutosha, ilui tumalize umasikini ukambani.

Kile kitu ingine nataka, ikiwa hii katiba ni ya kweli. Tangu Kenyatta alipokuwa mtawala, watu wanakanyagwa hapa na magari, watu karibu waishe. Kwa nini hawalipwi? Kwa nini hawalipwi? Watu wanakanyagwa na gari na hawalipwi. Ikiwa hii katiba ni ya kweli, hii magari inaitwa wa Coast Holias, mwenyewe anaitwa Kosla, Kosla akikanyaga mtu alipe. Ikiwa ni gari yako bus nimeingia na imeniuwa unilipe kwa sababu sikuwa nikiingia uniuwe. Mimi ni mzee wa kijiji, na mbwa ya matajiri ikiuma mtu, alipwi, tunataka alipwe kama kizamani.

Mimi narudi kwa nyinyi wanaume sasa. Wanaume wenzangu kama mimi. Mwanaume anaoa mwanamke, mimi nikimpa wewe mtoto wangu awe mke wako, wewe ukienda kunywa pombe, unakuja kuuwa jioni tu kama mbuzi. Nilikuwa nampa wewe uuwe. Hiyo katiba ikaangaliwe sana, sisi wanaume tunazoea sana kuuwa. Wewe unakuja nyumbani, mtoto nimekupa, nikulipa mthito yangu, unakwenda kugombana kidogo tu unauwa, na mimi ukilia peke yako, mimi nalia mimi na bibi yangu. Sasa utakiwi kuuwa mtoto wangu. (Interruption, Inaudible)

The question is huyu alisema kiswahi na mimi nikasema kikamba, okay. The question ni; when I was giving you my daughter as a mzee, I was not giving you my daughter to come and kill, I was giving you my daughter to care for you and you care for her also.

Tutarudia kikamba customary law, kama vile ule mzee amesema. Itawezekenaje, sasa mimi mzee nimempa wewe msichana wangu, kama nyinyi vile mnang'ara, na nikimpa wewe utaki kunilipa mahari, utaki kunilipa mahari. Inatakiwa ukichukuwa msichana ya mzee unalipa kabisa kama zamani vile tulikuwa tunalipa. Ya mzee ni hayo, basi asante.

**Com. Abida Ali:** Asante, na Wilson Ndulu, Wilson Ndulu, na jaribu kufupisha watu wamezidi sana.

**Wilson Ndulu:** Asante sana. Yangu ni mafupi kwa sababu mengi yamesemwa. Yale nilikuwa nafikiria imesemwa na wenzangu, wazee wale walitoka hapa, sisi wale watu tulikuwa kiapo ya Maumau. Nataka kufafanulia ma commissioners, vile

ilivyo. Mbeleni sisi watu wa Kenya, kitu cha kwanza tulikuwa tunatamani sana ni mchanga. Na yale mengine baadaye. Na wakati tulipochukuwa uwongozi wa Kenya, hatujapata hiyo. Ilifanyika hivi, ndio nataka kuwaeleze mkabadilishwe. Tunataka mabadiliko.

Wakati tulikuwa tunafukuza mzungu huko, tulikuwa tunataka mzungu aende, kwa sababu alikuwa amechukua haki yetu yote, ile imenona, ile mzuri. Na tukafukuzwa, tukapelekwe huko kwa milima kwenye mawe. Na wakati tulipochukuwa uwongozi, ikabadilishwa, matajiri ni watu wa serikali, basi tukakaliwa mara ingine. Ikawa acolony wengine, na ndipo ukaona sasa ukitembea huku, utakuta masikini wengi, kwa sababu hakuna ardhi ya kulima. Ardhi ile ilikuwa mzuri ya kulima, inakaliwa na marajiri. Kwa hivyo tunataka ibadilishwe.

Kile kingine, kuna mashamba mengine huko, na tunajua tunaelewa lease, wanapewa lease ya miaka 95 kalipokwishi, 95. Kwa hivyo tunataka hiyo ibadilishwe, wasipewe ingine, tugawiwe hiyo mashamba.

Kile kingine hapo hapo, kuna sheria ingine inatusumbua sana, inaitwa commissioner. Commissioner anawekwa mmoja Nairobi.

Kwa nini commissioner asiletwe district, watu wawe wakimwona. Sasa anawekwa huko, sawasawa yule mfalme alikuwa pale Mombasa, alikuwa anakwenda kuonekana huko, kwa sababu watu wanataka kuuza vitu huko na hawawezi kumwona. Kwa hivyo commissioners, ukiwauliza hawa watu wengi, awawezi kujua commissioner yuko wapi. Na huyo ana uwezo nzingi, nataka ipungunguzwe.

Wanainchi wawe wakipata mashambe rahisi, kwa sababu inchi hii ni yao.

Kile kingine nataka, wanainchi wote waliumbwa na Mungu, na wana Kenya wako hapa wa kiumbwa kila mtu na Mungu, apate kitu ya Kenya. Kwa nini watu wengine huko wanapewa acre tano, kwa nini watu wengine wanapewa acre mia moja na mia tano, kwa nini na sisi tumezaliwa hapa Kenya? Tumekuwa kuna watu wamezaliwa hapa Kenya, na wanaonekana labda wametoka inchi nyingine. Tunataka serikali ikijua watu wa Kenya aina moja, wakipewa kitu aina moja, isipokuwa elimu, unajua elimu iko tofauti na utajiri iko tofauti. Lakini mchanga yenyewe, kwa sababu ni wa inchi hiyo na sisi ni watu wa inchi hiyo, tunataka tupewe haki yetu ya mashamba.

Kile kingine, ni ya pili hiyo; tunataka mipaka ile ilikuwa imekaa mbeleni iangaliwe, iwekwe vile ilikuwa mbeleni. Kwa sababu ninajua mpaka wa ukambani na Maasai ulikuwa unatoka Embakasi, ukapita, ukienda mahali panaitwa Seinya, Seinya wakati wa Maumau, 1952 na 1953, wale watu wetu walikuwa wanafungiwa pale, walikuwa wanajulikana, wanafungiwa Machakos. Siku moja mimi nilienda uko, wakati wa Maumau, wale walikuwa wamefungiwa pale, na nikwauliza hapa ni wapi, ni umaasaini ama ni ukambani, ikawa ni Machakos. Ninamaanisha, ule mpaka ulisikia mzee mwenzangu alisema hapa Kwa Katue, ile mpaka ilikuwa kule, na tukasukumwa, mapaka sasa tukaanza kuambiwa ni barabara, iwe reli ya gari. Kwa hivyo mipaka iangaliwe, kama kila mtu apewe haki yake.

Tukitoka huko tunapitia mlima wa Chulu. Maovu iko sasa, ata mpaka uko pale. Na unakwenda mpaka mahali kunaitwa Ngulia, inashika ile mto. Tunataka mpaka wetu urudishwe hivi.

Kuna zingine.

**Com. Abida Ali:** Mzee jaribu ku summarise.

**Wilson Ndulu:** Kuna kingine, sisi tunataka katiba itengenezwe, ile ardhi ya serikali, ardhi ya serikali yote mahalu ilipo Kenya, ikipeanwa, wacha kupeanwa. Ni D.O na Chief. Wazee wahusishwe. Na upande huu, sisi tunasikia mahali fulani kunaitwa National Park, Forest, wazee wapewe nafasi ya kujua ni kitu gani kinaendelea huko. Kwa hivyo ninauliza commissioners, tafadhali nimalize imebakia kidogo. Nauliza sasa hii mpaka ikiwekwa, mpaka yetu na K.W.S, tuwe wazee na viongozi wenigne, tuwe tukijua, kwa sababu tunajua tukipeana National Park, tutapeana na condition. Kwa hivyo sisi hatuna condition na hao, tumewekana na hao.

Wacha niangalie kitu ingine.....

**Com. Abida Ali:** Asante mzee, wacha tupatie mtu mwingine nafasi. Chris Odhiambo? I will give you five minutes.

Chris Odhiambo: Asante sana. Jambo la kwanza nitaongea ni juu ya retirement. Naona ya kwamba ni vizuri kuwe na retirement ata kwa upande wa kisiasa, iwe mtu akifika umri ya miaka fulani asiwe anaweza gombea kiti yoyote ya kisiasa. Tuseme kama president, akifika umri wa miaka sitini, asiwe anaweza gombea kiti hiyo. Na pia tuseme ya kwamba naonelea wale ambao wame retire, civil servants ambao wameretire, wasigombee kiti yoyote ya kisiasa, maanake vijana wamesoma, hawana nafasi, ya kupata kazi kama hiyo. Kwa hivyo hawa wameretire waende nyumbani, waanze maendeleo ingine.

Kitu ingine ni juu ya citizenship. Hii uraia naona ya kwamba, inabaguwa wakina mama sana. Inabaguwa wakina mama kwa njia hii; tunakuta ya kwamba, mama akiolewa na mwanaume wa Kenya, huyu mama anakuwa raia, akitoka inchi ingine, anakuwa raia wa hapa Kenya. Lakini mwanaume, akioa mwanamke, akioa, I mean it is the other way round, I hope you understand. Inakuwa mwanamke (Interruption)

We understand what do you want to see in the constitution, we understand, what do you want to see?

Naona ya kwamba wapewe usawa. Mwanaume apewe uraia vile mwanamke pia anaweza pewa uraia upande wa kuowana.

Jambo lingine ni kuhusu mayors; hawa mayors wawe elected na raia, maanake ni viongozi wa raia.



Kitu ingine ni nomination; badala ya nomination, hawa wabunge kumi ambao wanakuwa nominated, kuwe na representation. Watu ambao ni walemavu, akina mama saa zingine, na vijana. Such cases, kuwe na representation badala ya nomination.

Nafikiri yangu ya mwisho ni president baada ya election. Kuwe na enough time ya kuapishwe, kusiwe president anachaguliwa, wiki moja ama siku tatu anaapishwa. Kuwe na kitu kama three months, kuwe na kitu kama three months, baada ya kuelektiwa ndio aapishwe. Hii ni muda ambao mtu kama alifanya magendo katika uchaguzi rigging, vitu kama hizo, huyo anawezakushtakiwa na asiwe president. Kwa hivyo kwa hayo, wacha ni malizie mwisho kwa wale wanaajiriwa. Waajiri naonna wanapatia watu saa zingine mshahara wa chini sana, bila kujali, huyu ni mtu wa familia na labda ni yeye peke yake ako kazini, ako na watoto watano, na anapewa below one dollar. Hii ni pesa kidogo ambayo iwezi tosheleza labda ata watu wawili.

Kwa hivyo kuwe na salary basic, chini kidogo, minimal iwe ni kitu kama three dollars ama kitu kama ambayo inaweza tosheleza familiy, ata kama ana mtoto mmoja. Kwa hivyo ni hayo tu, asanteni.

**Com. Abida Ali:** Felix Mataka.

**Felix Mataka:** The commissioners, ladies and gentlemen. I am first going to talk about the pension, the pension Act. I think the present pension, which only allows the pensioner to get the pension, and after he dies the widow doesn't get the pension.. I think that one should be abolished, so that when the pensioner dies, the widow or the widower should continue getting pension , because, he or she has not died.

The next thing is about education. Presently we have many children on the streets and also in the rural areas, who have finished primary education and they have no where to go, and the number is still growing. So, I would like to request you commissioners to take note that we would like the constitution to provide for those children who are jobless. Because they are very many and the number is also increasing. And, the education given to our children should also be free, in the government institute. That is, universities and also when they finish the education, the training, the courses should also be free because many of our children are finishing form four with problems of fees and then when they apply for courses, you find these courses are so expensive. So, I think if they cannot be free courses, let them be given loans, like the universities, so that the children of the poor should get loans to attend this courses.

The other one is this land problem. It is a sensitive problem and for one thing I would suggest that; there should be no any nothing like squatters. Because where there is land, government land, and there are people called squatters, why can't they be given that land. What is this land being reserved for? I think such a land is likely to be grabbed by the able person, and I also think in distribution of land, those who are able to buy land and all that have bought land and are able should not be given land. Sometimes civil servants who are big bosses are rewarded with land, and they have land and they are able to buy land. They are given land and a poor person without land is being called a squatter. He fails to understand why he is not given land and why are the others, why are civil servants, who have been getting salaries are on top given free land.

Now, the next thing is about election. The election commission should be independent, so that it can prosecute those who violate the regulation immediately.

About presidential election; I think as somebody suggested, it should be in the calendar so that we know such and such a date, is when election is there, so that it is not used as a secret weapon.

**Com. Abida Ali:** Please summarize.

**Felix Mataka:** And, the last thing I would say is the Attorney General, the Chief Justice should be elected by the parliament. Names should be presented to parliament who will get them and present them to the appointing authority. Thank you.

**Com. Abida Ali:** Thank you very much. Joseph Kiamba. Five minutes please.

**Joseph Kiamba:**

**Translator:** Mimi nitasema Kikamba kwa sababu mimi ni mkamba. Mimi nitasema juu ya shamba ambayo ninayokanyaga. Nimesikia point nyingi ambazo zimetolewa na watu wakitafuta mashamba. Lakini ile shamba ambayo tunauliza habari yake bado haijafikiwa kulingana na maoni yangu. Kwa sababu hapa kwetu mtu akikufa, kuna mchanga ingine hapa chini unachukulia permit ya kuzika. Nauliza shamba tupewe yote, kutoka hapa top mbaka chini, underground. Na tupewe in the atmosphere, pahali mimi napakana na Mungu. Ikiwa mimi ni mwanakenya wa kweli. Na hiyo sehemu iwe yangu na yangu kabisa. Ikiwa kutakuja kupatikana kitu chochote ambacho kitatajikana na serikali hapo ndani, ninatakiwa niombwe, niuze hiyo sehemu ya inchi yangu kulingana na market value of the land by then. Na nikisha uzia serikali hiyo sehemu, wao wanibadilishie na kunijengea sehemu ingine mzuri, nyumba kama ile yangu, na sehemu ingine mzuri kama yangu. Ikiwa hii shamba ni yangu kweli.

Nitarudia mambo ya election. Ile election ambayo itakuja, na ikiwa tutapata serikali ingine mpya, wacha hii tuko nayo sasa. Mwanainchi aangaliwe vizuri na serikali kwa sababu mwanainchi bado hajatambuliwa na serikali vizuri. Kwa sababu nasika kuna sehemu inaitwa private land, kwa sababu duwa ni private land. Ukipitia, ukifika hapa kwa shule inaitwa St. Joseph, kufikia gate ya dua, kuna kibao inaandikwa 'No Entry bila permit' na uwezi pitisha mtu wako hapo bila kuwa na permit. Ikiwa unatoka Masonga, mpaka uzunguke Kitui road. Hii inchi nauliza ndio yangu? Tunaomba pia hii neno inaitwa 'Trespass' iondolewe katika Kenya. Kwa sababu Kenya ni yetu na there should be no one better person than the other in this country.

Ile ingine nitasema ni juu ya Kenya's Wealth Division. Sisis tunaishi katika settlement scheme na sisi tunalipa one acre, 2,500/=.

Na sisi ni wale tulifukuzwa kwa milima ya Chulu hills na wengine Kalembwani. Na hatujapewa compensation, what are we really paying for? Niliwacha shamba kubwa sana kule Chulu Hills, hapa nimepewa ka shamba kadogo, ka acre tano, sasa mimi nalipa 25,000, na niliwacha shamba kubwa nikafukuzwa.

Tuliwacha shule, makanisa, mashamba yetu, kila kitu ambayo uwa owned by a normal citizen tuliwacha Chulu Hills. Naomba watu walifukuzwa Kalembwani, Chulu Hills, serikali itakayokuja baada ya kutengeneza hii katiba, ifikirie kupatia sisi compensation, kwa sababu tuliwacha kila kitu.

The last view, nitasema juu ya Provincial Administration. Nitasema kiwango kufikia District level, kwa sababu mimi ufika hapo.

Nilipokuwa nikiangalia habari ya wilaya, sijaona kazi ya D.C. Sioni kazi ya D.O hata I don't know his work. Mtu mimi najua kazi yake ni Chief na Assistant Chief. Sasa tena nikiangalia kwa ndani zaidi, hawa ma Assistant Chiefs wamekuwa very senior kabisa, Village Elders ndio wafanyi kazi wa serikali. Assistant Chief amekuwa mkubwa, anakaanga kwake nyumbani, wazee wa Village Elders wanaleta repoti kwake, as if yeye ni governer. The Village Elder is neve counted as a useful person for his duties that he does. Na most of the work done on the line of adminstration is done by the Village Elder. We are always on the low level with Village Elders, it being a funeral, it being development, school construction, anything, we are always low with Village Elders. I would like after this constitution we are making, A village Elder to be put on salary and let his salary come from the consolidated fund. Mimi Kiamba, thank you very much.

**Com. Abida Ali:** Asante sana. Francis Maina? George Mulei? Oh ni wewe asante. Lakini ongea na Kiswahili.

**George Mulei:** Mimi kama wengine, commissioners nashukuru sana. I have written my report but I would give some highlights.

I will start with a preamble. It is my humble request that there be a preamble in kenya's constitution, and let it remember our freedom fighters. Let it also mention something to do with our time. When we moved from the colonial time up to independence.

My second point is about direct principles on state policy. Kenya's economy has been eaten away by professionals failing to adhere to their professional ethics, for example, doctors, engineers, on roads and so forth. It is my view that if a professionalist fails to go to his professional ethics, he be made to pay for the damages cost by negligence and this should go down to the law so that such professionalist should be prosecuted.

My third point is no constitutional supremacy. It is my humble submission that the kenya's constitution be below the people, the people should be above the constitution.

The other thing is about, defence and the national security. We should have what we call, a National Security Council to discipline the armed forces, and when there is emergency or war or national disaster, let it be declared by the parliament not by the president alone.

